SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 3

**MANYONI** yachanja UVIKO-19, asilimia 81 lengo lililowekwa




Nipashe
Alhamisi Desemba 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580810
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Fisi wawa tishio kwa wanafunzi

**WADAI** kuhofia kupoteza maisha wanapokwenda shuleni na kurudi, waiangukia serikali... *Endelea ukurasa 10*

**DARASA**



Mwonekano wa darasa la shule shikizi katika kitongoji cha Imalange, Kijiji cha Kabanga, Ushetu wilayani Kahama, Shinyanga, linalotumiwa na wanafunzi wa darasa la awali, kwanza na darasa la pili kabla ya kuhamishiwa katika Shule ya Msingi Kangangangа kuendelea na darasa la tatu. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Waombaji 22,000 wajitokeza ajira 350 TAKUKURU

UKURASA 2

## Mke afurahia mume wake kufungwa maisha gerezani

UKURASA 2

**MICHEZO** PABLO ACHAMBUA KUNDI LA SIMBA CAF UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

## Mapigano wakulima, wafugaji yasababisha kifo na majeruhi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MAPIGANO yamezuka kati ya wakulima na wafugaji wilayani Malinyi mkoani Morogoro na kusababisha kifo cha mkulima mmoja na wengine sita kujeruhiwa.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea katika mradi wa kilimo cha umwagiliaji uliopo kijiji cha Itete, akimtaja aliyepoteza maisha kuwa ni Abdul Said (34) mkazi wa Ifakara wilayani Kilombero.

Kamanda Muslim alisema tukio hilo limetokea Desemba 27 mwaka huu huku chanzo cha mapigano hayo ni baada ya vijana watatu akiwamo Abdul kuzuia mifugo iliyoingia katika mashamba hayo.

Alisema wakati vijana hao wakiendelea kuzuia mifugo hiyo ndipo yalipozuka mapigano baina yao na wafugaji hao, kwamba walizidiwa nguvu na kukimbilia kusikojulikana kisha mwili wa kijana huyo ulipatikana kesho yake usiku.

"Baada ya kutokea mapigano hayo wale wakulima walizidiwa nguvu, hivyo wakakimbia, Jeshi la Polisi Malinyi lilipopata taarifa lilianza jitihada za kuwatafuta bila mafanikio hadi ilipofika saa 9 usiku ndipo mwili huo ulionekana katika mashamba hayo," alisema Muslim.

Kamanda Muslim alisema kuwa baada ya mwili wa kijana huyo kupatikana akiwa amefariki baadhi ya wanakijiji walilazimisha uchunguzi wa kidaktari kufanyika hadharani, ndipo daktari alipofika na kuufanyia uchunguzi.

Aliendelea kueleza kuwa baada ya uchunguzi kukamilika daktari alishindwa kutoa majibu hadharani kwa sababu za kimaadili, ndipo wanakijiji hao wakaanza kuwashambulia kwa mawe daktari na askari waliokuwa sehemu ya tukio.

Kamanda Muslim alisema baada ya kutokea kwa hali hiyo Jeshi la Polisi lililazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wanakijiji hao.

"Jeshi la Polisi lililazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wanakijiji hao baada ya kuanza kurusha mawe kushinikiza ripoti ya uchunguzi wa daktari isomwe, baada ya kutawanyika baadae Jeshi la Polisi tulirudi kuangalia ndipo tukapata taarifa kuwa kuna makazi ya wafugaji 17 waliokuwa wakiishi jirani na mashamba hayo yamechomwa moto," alisema Kamanda Muslim.

Alibainisha kuwa katika tukio hilo la uchomaji moto wa makazi hakuna madhara yeyote kwa binadamu yaliyotokea kwa sababu wafugaji hao walikuwa wameyakimbia makazi yao baada ya kuona kuna mkusanyiko mkubwa wa watu kijijini hapo.



Rais wa Zanzibar ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi zawadi mwanafunzi bora wa Shahada ya Sayansi ya Kompyuta, Omar Saleh Suleiman, katika mahafali ya 17 ya chuo hicho, yaliofanyika Ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein Tunguu Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: IKULU**

## Mke afurahia mume kufungwa maisha gerezani

**Na Said Hamdani,** LINDI

ADHABU ya kifungo cha maisha gerezani aliyohukumiwa Selemani Matola (53) kwa kosa la kumnajisi mjukuu wake mwenye umri wa miaka minane, imeibua shangwe kwa mke wake Somoe Yusufu (42), aliyesema imemfariji.

Somoe ambaye ni mke wa ndoa wa Matola, alitoa kauli hiyo wakati wa mahojiano na mwandishi wa habari, baada ya hukumu ya mumewe.

Hukumu hiyo ilitolewa Desemba 24, mwaka huu katika Mahakama ya Wilaya ya Lindi baada ya Matola kupatikana na hatia ya kumnajisi mjukuu wake wa kike anayesoma darasa la kwanza.

Tukio hilo liligundulika baada ya mke huyo kumfuma mume wake chumbani kwa wajukuu wao, akifanya unyama huo.

Somoe alisema, kimsingi amefarijika na adhabu aliyopewa mumewe na kwamba hajutii adhabu aliyopewa, licha ya kuwa ni mume wa ndoa aliyezaa naye watoto wanne na wajukuu wawili.

"Kwa unyama uliofanywa na huyu mwanamume, wala sijutii, badala yake nimefarijika kupita maelezo," alisema Somoe.

Akisimulia jinsi alivyofanikisha kumkamata mume wake huyo, alisema Desemba 17, mwaka huu usiku, alimuaga mumewe kwamba anaenda kushiriki ngoma ya unyago ya watoto wa kaka yake, huku nyumbani akiwaacha watoto akiwamo mjukuu wao na mume wake.

Alisema ilipofika usiku wa manane aliamua kurejea nyumbani na alipoingia chumbani kwao, aliona mabadiliko ikiwa ni pamoja na watoto wao kuwakuta wamelazwa kitandani kwao, huku mume wake akiwa hayupo, hali iliyoanza kumpa maswali mengi.

Alisema baada ya kujiuliza, aliamua kwenda chumba kinachotumika kulala watoto, na kufanikiwa kumkuta mume na mjukuu wake kitandani, huku wakiwa utupu kama walivyozaliwa na alipowakagua kwa kuwamulika tochi akabaini jambo.

"Niliwakuta wamelala tena fofofo niliwasha tochi nikaona mbegu za kiume mapajani mwa mjukuu wetu, nikaona tayari kuna biashara imefanyika," alisema Somoe.

Baada ya kubaini hali hiyo, alisema alitoka nje na kuita majirani na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji chao, Issa Juma, ambao walifika nyumbani na kumkuta akiendelea kuuchapa usingizi, na kuamua kumuamsha na kumfikisha ofisi ya kijiji kata na baadaye polisi.

Somoe aliwaomba wanawake wenzake kutokubali kufumbia macho wanapowabaini waume zao kufanya vitendo vya kinyama dhidi ya watoto wasio na hatia na kuwafikisha mikononi mwa vyombo vya sheria kwa hatua zaidi ili kukomesha unyama unaofanywa na baadhi ya wanaume.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Juma amepongeza hatua iliyofanywa na mama huyo na kuwa ni mfano wa kuigwa na wanawake wengine katika kuondoa au kupunguza vitendo vya unyanyasaji dhidi ya watoto wasio na hatia. Ofisa Mtendaji Kata ya Kiwalala, Zaituni Lichinga, naye alimsifu mwanamke huyo na kusisitiza kama wanawake wote wangekuwa na msimamo kama wa Somoe, vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wasio na hatia vingepungua kama sio kumalizwa kabisa.

Desemba 24, Mahakama ya Wilaya ya Lindi, kupitia Hakimu Mwagala Muyonga, ilimhukumu Matola kifungo hicho na kumlipa mtoto huyo fidia ya Sh. 3,000,000.

## Waombaji 22,000 wagombea nafasi ajira 350 TAKUKURU

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya watu 22,106 wanatarajiwa kushiriki usaili wa maandishi wa kuomba nafasi za ajira za maofisa uchunguzi na maofisa uchunguzi wasaidizi 350 zilizotangazwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), utakaofanyika kwenye vyumba vitatu jijini Dodoma. Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na TAKUKURU jana, jumla ya watu 12,377 wanaomba nafasi 200 za maofisa uchunguzi zilizotangazwa.

Pia waombaji 9,729 wanaomba nafasi 150 za wachunguzi wasaidizi wa TAKUKURU na wote watatakiwa kushiriki usaili wa maandishi Januari 8 mwakani.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, waombaji hao watatawanywa kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo cha Mipango na Chuo Kikuu cha St. John.

Kwa mujibu wa mgawanyo wa waombaji hao, chumba kitakachokuwa na waombaji wachache ni 200 huku cha juu kikiwa na 1,500.

Taarifa iliyotolewa jana kwenye mitandao ya kijamii na tovuti rasmi ya taasisi hiyo na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, bosi huyo anawataka waombaji hao kufika eneo la usaili Januari 8 mwakani na kwamba mtihani wa waombaji wa nafasi ya Ofisa Uchunguzi utaanza asubuhi.

Alisema kwa nafasi ya Ofisa Mchunguzi Msaidizi mtihani wake utaanza saa 6:00 mchana, siku hiyo hiyo, huku wote watakiwa kujaza fomu zenye taarifa binafsi kwenye taarifa iliyopo kwenye orodha ya majina na watatakiwa kuikabidhi siku hiyo.

"Waombaji walioitwa kwenye usaili huu wahakikishe wanachukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 muda wote wanaposafiri na wanapokuwa kwenye chumba cha mtihani," alibainisha katika taarifa hiyo.

TAKUKURU kupitia taarifa hiyo pia ilibainisha kuwa watakaofaulu kwenye mtihani wa maandishi ndiyo watakaoitwa kwenye usaili wa mahojiano.

Hali hii iliwahi kujitokeza kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) ilipotangaza nafasi 900 za ajira na waombaji walijitokeza zaidi ya 10,000 na kulazimu kufanya usaili kwenye Uwanja wa Taifa (sasa unaitwa Uwanja wa Mkapa) mkoani Dar es Salaam.

Hata hivyo, wadau mbalimbali wamekuwa wakikosoa utaratibu huo na kuzitaka mamlaka kutumia mfumo wa kompyuta kuchambua waombaji na kupata wachache wa kuwapitisha kwenye usaili kuliko kuwaingiza gharama mamia kwenda kufanya usaili na kuingia gharama kubwa za malazi, chakula na nauli.

## HABARI KITAIFA

# Manyoni yachanja 81% UVIKO-19

**Na Mary Geofrey,** MANYONI

HALMASHAURI ya Itigi, wilayani Manyoni mkoani Singida, imefanikiwa kutoka asilimia 81 ya dozi 7,294 za chanjo UVIKO-19 walizopokea.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itigi, Dk. Emmanuel Mallange, aliyaeleza hayo jana mbele ya maofisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Victorina Ludovick, walipotembelea halmashauri hiyo katika kuhamasisha utoaji wa chanjo.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19, katika Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili, unaotekelezwa na wizara hiyo, kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma.

Dk. Mallange alisema, dozi hizo zilijumuisha Johnson and Johnson asilimia 92, Sonopharm asilimia 70 na Pfizer asilimia 88.

Alisema pia watumishi 53 kati ya 90 walipewa elimu ya UVIKO-19 kurahisisha huduma za chanjo katika halmashauri hiyo.

Alisema pia wamefanya mikutano ya uhamasishaji katika kata tisa za halmashauri hiyo na kufanikiwa kuchanja watu 757.

Alitaja changamoto zinazokwamisha juhudi za watumishi katika kuwafikia wananchi wengi zaidi ni uhaba wa mafuta, posho za kujikimu kuwa ndogo, mwitikio mdogo wa wananchi na upungufu wa watumishi wa afya katika baadhi ya vituo.

Dk. Mallange alisema wamejiwekea mikakati ya kuhakikisha wanafikia malengo waliyopewa kwa kuendelea kuongea na wadau ili kutatua baadhi ya changamoto.

Alisema pia wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19 kuomba vibali vya ajira ili kuongeza watumishi na kupeleka pikipiki katika vituo ili kusaidia kutoa huduma.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Ufuatilia na Udhibiti wa Magonjwa, kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, aliipongeza halmashauri hiyo kwa jitihada kubwa wanazofanya za kusogeza chanjo kwa wananchi.

Alisema halmashauri hiyo imefanya vyema katika kampeni hiyo, hali itakayosaidia Mkoa wa Singida kupiga hatua kubwa katika kufikia lengo la kuchanja watu 3,000 kila siku.

Malengo ya serikali ni kila mkoa kuchanja watu 4,000 kwa siku na watu 80,000 hadi 100,000 kila siku kitaifa.

Mkakati huo unalenga kufikia asilimia 60 ya Watanzania wote wanaotakiwa kupata chanjo ya UVIKO-19 nchini.



Kamanda wa Kikosi cha 511 cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kanali Amani Siyani (kushoto), akimkabidhi msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo chakula mwanzilishi wa kituo cha kulelea watoto cha Uhai Development Organization (UDO), Teddy Kachwande, kwa ajili ya matumizi ya watoto wanaolelewa katika kituo hicho wakati maofisa na askari wa kikosi hicho walipotoa misaada kwa vituo vitatu vya kulelea watoto kikiwamo kituo hicho na kituo cha Kind Hearth Afrika na Tankids Coming Home jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mawakili wakwamisha kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JOPO la mawakili sita wa upande wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, limekwamisha kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo baada ya kushindwa kufika mahakamani.

Sabaya na washtakiwa wenzake sita; Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31), wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Jana mahakama hiyo ilitarajiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa na upande wa utetezi, wakipinga shahidi wa 13 wa Jamhuri, Ramadhani Juma (39) kutoa ufafanuzi kuhusu video za CCTV zinazowaonyesha vijana wanaodaiwa ni wa Sabaya wakiingia Benki ya CRDB Tawi la Kwa Murombo jijini Arusha na kukabidhiwa fedha kiasi cha Sh. milioni 90.

Akizungumza mahakamani huko, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai kwa kuwa mawakili wa washtakiwa wote hawakuhudhuria katika usikilizwaji wa shauri hilo, mahakama hiyo haiwezi kutoa uamuzi wa pingamizi hilo kwa kuwa washtakiwa hawatakuwa na uwakilishi.

"Mheshimiwa hakimu, mawakili wa washtakiwa hawajafika hata mmoja mahakamani, lakini washtakiwa wapo wote. Kwa kuwa wawakilishi hao hawapo, mahakama haiwezi kutoa uamuzi.

"Sheria imeelekeza wazi ili kesi iweze kuendelea au kusikilizwa labda washtakiwa wawe wametoa uwakilishi wa mawakili wao, hivyo kwa kuwa mawakili hawajafika mahakamani, tunaiomba mahakama itupangia tarehe nyingine kwa ajili ya uamuzi mdogo," alidai.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinda, aliwahoji washtakiwa hao kama bado wanawakilishwa na mawakili hao na walithibitisha kwamba uwakilishi wao unaendelea katika kesi hiyo.

Baada ya washtakiwa hao kutoa majibu hayo, Hakimu Kisinda aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 3 mwakani itakapoendelea kusikilizwa katika mahakama hiyo.

Desemba 17, mwaka huu, mawakili wa utetezi, wakiongozwa na Silvester Kahunduka, walipinga mahakamani huko shahidi huyo kutoa ufafanuzi kuhusu video hizo, wakidai kwamba hakuhusika kuziandaa.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote; shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linalomkabili mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) peke yake; na shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake na shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linalowakabili washtakiwa wote saba.

Inadaiwa kuwa Februari 22, mwaka huu, Sabaya kwa kushirikiana na wenzake, wakiwa katika eneo la Kwa Murombo jijini Arusha, walijipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90, wakitambua kwamba kufanya hivyo ilikuwa ni zao la vitendo vya rushwa.


## BARRICK GOLD MINE
### BULYANHULU, KAHAMA
## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **BARRICK GOLD MINE,** Bulyanhulu, Kahama watauza kwa mnada wa hadhara Mitambo mbalimbali na magari chakavu Jumamosi tarehe 8 Januari, 2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika katika eneo la mgodi wa Barrick Bulyanhulu – Kakola.

**MALI ZITAKAZOUZWA:**

| Idadi | Aina | Hali ya Mtambo | Ushuru |
|---|---|---|---|
| 9 | Heavy Duty Dumping Trucks | Chakavu | Haujalipwa |
| 22 | Work Platform Machine | Chakavu | Haujalipwa |
| 4 | Forklift | Chakavu | Haujalipwa |
| 4 | Hydraulic Mobile Crane (Mine) | Chakavu | Haujalipwa |
| 7 | Wheel loader & CAT Grader | Chakavu | Haujalipwa |
| 73 | TOYOTA L/cruiser HardTop, PickUps & S/Wagon | Chakavu | Haujalipwa |
| 2 | Scania Concrete mixer/Bowser | Hafifu | Haujalipwa |
| 4 | M/Benz, TATA, KW Truck, Magrius & Nissan Trucks, Crane, MiniBus & Concrete mixer | Hafifu | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa kwenye eneo la mgodi wa Barrick Bulyanhulu – Kakola. Kuanzia tarehe 5 hadi 7 Januari 2022 Saa 3:30 asubuhi mpaka Saa 10:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi awe amesajiliwa kama "mnunuzi na muuzaji wa vyuma chakavu" na kupata Kibali cha NEMC.
2. Mshiriki atatakiwa kulipa Commitment Fee Tsh. 50 Million kwenye A/C ya Barrick No. 100542048, Citi Bank, Swift: CITITZTZ jina la A/c ni BULYANHULU. Fedha hii itakuwa ni sehemu ya malipo au itarejeshwa kwa aliyeshindwa.
3. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi (kabla ya 14-Jan-2022) katika bank Akaunti ya Barrick utakayoelekezwa, ukishindwa kulipa kwa muda huo mali itauzwa tena na dhamana haitarudishwa.
4. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana yeyote.
5. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru kama atakavyokadiriwa na Mamlaka ya TRA.
6. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mali aliyonunua baada ya kulipa malipo yote na kodi kabla ya tarehe 22 January 2022 kwa gharama zake.
7. Kila mtu atakayeingia kwenye Mnada atatakiwa kuwa na Bid no: itakayopatikana mlangoni baada ya kuonyesha Bank slip na kibali cha NEMC.
8. Kila mshiriki atatakiwa avae PPE, barakoa na kutumia kitakasa mikono wakati wote.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE , SIMU NA: +255 754 284 926,**

# RC aingilia kati kuzuia ma-DC kung'oa mazao

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewataka wakuu wa wilaya mkoani humo kusitisha kung'oa mazao ya wakulima waliochanganya pamba na mahindi kwa hofu ya ukame.

Ameagiza wawaache kwa sasa lakini msimu ujao wasisitizwe kufuata na kuzingatia kanuni na sheria za zao hilo.

Kafulila aliagiza hayo jana wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Bariadi mjini Bariadi.

Alisema kuwa mbali na elimu iliyotolewa kwa wakulima juu ya kutochanganya pamba na mazao mengine, bado kuna wilaya ambazo wakulima wake wameendelea kufanya hivyo kwa hofu ya kupatwa na njaa kwa msimu huu kutokana na uhaba wa mvua.

"Inaonyesha kampeni iliyofanywa na balozi wa pamba na viongozi wa wilaya na mkoa ya namna bora ya kushiriki kilimo bora ilieleweka lakini baadhi ya maeneo imekuwa tofauti.

"Na kutokana na mkoa wetu kutangazwa kuwa ni miongoni mwa mikoa itakayokabiliwa na uhaba wa mvua, wakulima wakaingiwa na hofu na kuamua kuchanganya mazao," alisema.

Kafulila alisema kuwa kwa kuzingatia yote hayo, serikali imeona kuna haja ya kuwasamehe wakulima hao waliofanya hivyo kwa msimu huu wa mwaka 2021/22 waachiwe, lakini idadi yao lazima ichukuliwe na msimu ujao waone kama watajirekebisha na kufanya vizuri.

Mbunge wa Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, alimshukuru mkuu wa mkoa kwa uamuzi wake wa kuwasamehe wakulima hao, lakini maofisa ugani waendelee kuwaelimisha wakulima hao.

Aliongeza kuwa kitendo cha viongozi kung'oa mazao ya wakulima ambao wamefanya hivyo kwa kujihami na janga la njaa, ni kutengeneza chuki baina ya wakulima hao na serikali.

Sambamba na hilo, mbunge huyo alimshauri mkuu wa mkoa kufuta kesi 14 za wakulima waliofunguliwa kwa kosa la kuchanganya mazao hayo ili kuwapa fursa na muda wa kujutia na kujirekebisha.

Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba nchini, Marco Mtunga, alipoulizwa juu ya uamuzi huo, hakuwa tayari kulizungumzia hilo.




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, Yusuph Kamota, akisaidia kusukuma daladala iliyokuwa imezimika ghafla eneo la Miyomboni kwenye barabara kuu ya Iringa-Dodoma juzi. PICHA: FRANCIS GODWIN

## Jela miaka 11 wizi wa kuvunja

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu mkazi wa Mmongo, Manispaa ya Lindi, Haji Abdallah Mazoea (49) kifungo cha miaka (11) jela baada ya kupatikana na kosa la kuvunja nyumba na kuiba mali yenye thamani ya Sh. 1,503,000.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Batraine alimuuliza mshtakiwa kama ana sababu za msingi zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kwa kesi inayomkabili.

Mshtakiwa alijetetea kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na alilazimika kufanya hivyo kutokana na ugumu wa maisha.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Rabia Ramadhani, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake kwa madai ni mwizi mzoefu, anayehatarisha usalama wa mali za watu wengine wanaotafuta kwa kutumia jasho.

"Mheshimiwa hakimu taarifa ambazo ofisi yetu inazo mshtakiwa ni mwizi mzoefu hapa kwetu Lindi, watu wengi wanmlalamikia huyu mshtakiwa kwa vitendo vyake vya wizi," alidai Rabia.

Hakimu Batraine akitoa hukumu hiyo alisema kosa la kuvunja, atatumikia kifungo cha miaka saba na la kuiba atakaa jela miaka minne na kufanya jumla ya miaka kuwa 11.

Alisema kwa kuwa adhabu zinakwenda kwa pamoja mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka saba gerezani.

Awali, ilidaiwa na mwendesha mashtaka wa serikali Rabia Ramadhani kuwa mshtakiwa akiwa anatambua anachofanya, Septemba 21, mwaka huu, huko mtaa wa Amani katika Manispaa ya Lindi, alivunja nyumba ya Rose Osward Condrard na kuiba bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Sh. 1,503,000.

# Majaliwa: Watoto ni wenu, lakini kwenda shuleni lazima

**Na Mwandishi Maalum,**
NACHINGWEA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema jukumu la kulea watoto na kutafuta mahitaji ni la wazazi, lakini wajibu wa kuwasomesha watoto hao ni wa serikali.

"Tulishasema mtoto wa Kitanzania kwenda shule ni lazima. Watoto ni wao, lakini kwenda shule ni lazima. Ndiyo maana serikali ilifuta ada katika shule zote," Majaliwa alisema hayo juzi alipozungumza na viongozi wa Mkoa wa Lindi waliofika kumpokea kwenye Uwanja wa Ndege wa Nachingwea mkoani humo.

Waziri Mkuu alisema ujenzi wa madarasa unaoendelea kote nchini hivi sasa unalenga kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anakwenda shule iwe ni ya msingi au ya sekondari.

"Tunataka tuondoe kabisa tabia ya kukuta watoto wetu wakifanya biashara kwenye stendi za mabasi au nyumba za starehe," Majaliwa alisema.

Waziri Mkuu pia aliwataka viongozi hao wawahimize wananchi watunze akiba ya chakula walichonacho kwa sababu Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa mikoa ambayo bado haijaanza kupata mvua ya vuli.

"Lindi ni miongoni mwa mikoa ambayo haijapata mvua hadi sasa. Lazima tujipange, tuangalie kwani yako mazao ya kibiashara na yako pia mazao ya chakula ambayo yanatumika kibiashara. Tutunze akiba tuliyonayo, tusitumie akiba hii kutengeneza pombe au kufanyia sherehe," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Tellack, alisema mkoa huo umekamilisha mauzo ya korosho isipokuwa kwa maeneo machache na wamefanikiwa kuuza tani Sh. milioni 63 zenye thamani ya Sh. bilioni 131.

Kutokana na taarifa hiyo, Waziri Mkuu aliwataka viongozi wa mkoa na wilaya wabebe jukumu la kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwekeza kwenye miradi mbalimbali badala ya kutumia fedha hizo kwa starehe.

"Hatuwezi kuwafundisha watu namna ya kutumia fedha yao, lakini tunao wajibu wa kuwaelimisha. Tutoe miongozo ili wafanye uwekezaji, wajenge nyumba bora za kuishi, wanunue vifaa ili watoto waende shule na wajali afya zao," alisema.

Waziri Mkuu yuko jimboni kwake Ruangwa kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka.

# Waziri aonya mifumo ya kizamani TAZARA

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Godfrey Kasekenya, ameutaka uongozi wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) kubadilisha mtazamo na kwenda kibiashara, vinginevyo wataendelea kulididimiza na kuua mamlaka hiyo.

Amesema menejimenti na wafanyakazi wa TAZARA ili kuliinua shirika hilo wanapaswa kubadilika kiutendaji sambamba na mifumo imara ya kiuendeshaji.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozuru katika mamlaka hiyo kwa lengo la kujifunza na kufahamu matatizo mbalimbali yanayoikabili. "Ninawaeleza ukweli hata mkiletewa mabehewa mapya, vichwa vya treni vipya, miundombinu ikikarabatiwa, lakini kama hamtabadilika kimtazamo, mtaishia kufeli kila siku.

"Bado hamjawa na mawazo ya kibiashara, kama hamtabadilika, mtaendelea kukwama, kuna haja ya kufanya marekebisho makubwa ili TAZARA itembee," alisema.

Kasekenya alihoji mfumo wa ukusanyaji mapato unaotumiwa na mamlaka hiyo, huku akiwaonya kwamba endapo wasipotumia mfumo wa elektroniki, wasitarajie kufanikiwa.

Kasekenya alihoji: "Mnakusanyaje mapato yenu? System (mfumo) wenu ukoje, manually au automatically? Kwenye vituo vya treni mnakusanyaje mapato? Yawezekana mnamnufaisha mtu mmoja. Ninawaeleza kama hamkusanyi kielektroniki mtakwama tu na mtaendelea kupata hasara."

Kaimu Mkurugenzi wa TAZARA, Christopher Shiganza, alisema TAZARA inakabiliwa na matatizo mengi ya kiuendeshaji ikiwamo uchakavu wa madaraja.

Alisema TAZARA pia inakabiliwa na madeni lukuki yanayokaribia dola za Marekani milioni 181.2, mtaji mdogo na uhaba wa wafanyakazi. "Licha ya changamoto zinazotukabili lakini tunatarajia kukarabati mabehewa zaidi ya 100 kupitia fedha za serikali. Tunaomba msaada wa serikali Sh. bilioni 14.9 kwa ajili ya kulipa mishahara wafanyakazi," alisema Shiganza.

Baadhi ya wafanyakazi walihudhuria kikao hicho, akiwamo Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli (TRAWU), Jackob Shiduka, alisema ushirikishwaji wa wafanyakazi wa TAZARA kwenye uamuzi mbalimbali haupo.

Alisema wafanyakazi wamekuwa hawapewi taarifa zozote kutoka kwa menejimenti. Alisema miundombinu ya reli ni chakavu sambamba na wafanyakazi kudai malimbikizo ya mishahara.

Mfanyakazi mwingine, Kalunde Mohammed, alisema: "Tunaomba serikali itupatie mtaji, itupatie mabehewa, vichwa vya treni, vipuri pamoja na mtaji. Serikali iwekeze zaidi kwenye sekta ya reli sambamba na kuwahamasisha wafanyabiashara kutumia reli kusafirisha mizigo yao badala ya barabara."



Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini mkoani Tanga (RUWASA), Upendo Magongo (katikati), akiwa na makandarasi katika zoezi la utiaji saini miradi ya maji jana katika ukumbi wa mkuu wa mkoa, wa kwanza kulia ni Mhandisi Fidelis Bachwa wa kampuni ya FHS Engineering Ltd. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Mbaroni tuhuma kukutwa na nyara za serikali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha, linamshikilia Langidari Laizer (22), mkazi wa Kisongo wilayani Monduli kwa tuhuma za kukutwa na swala saba akiwa amewahifadhi kwenye mifuko miwili ya salfeti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema jana mbele ya waandishi wa habari jijiji Arusha kuwa mtuhumiwa huyo alitiwa mbaroni juzi na polisi majira ya saa 10:00 usiku katika kijiji cha Maserani kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori.

"Baada ya kupata taarifa za kintelijensia, tuliweka mtego na kufanikiwa kumtia mtuhumiwa huyo mbarani majira ya saa 10;00 huko katika kijiji cha Maserani, wilaya ya Monduli akiwa na swala saba akiwa amewahifadhi kwenye mifuko miwili ya salfeti," alisema.

Kamanda Masejo alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na polisi kwa mahojiano zaidi na upelelezi ukikamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Kamanda Masejo alitumia fursa hiyo kuwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa Polisi dhidi ya uhalifu na wahalifu wanaofanya vitendo mbalimbali vikiwamo vya ujangili ili kuendelea kuimarisha amani na utulivu katika mkoa.

**SHEREHE MWAKA MPYA**

Kuhusu sherehe za Mwaka Mpya, Kamanda Masejo alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama limejipanga vyema kuhakikisha Sikukuu hiyo inasherehekewa kwa amani na utulivu.

Alisema wamejipanga kuhakikisha nyumba za ibada, kumbi za starehe na maeneo mengine yanakuwa na ulinzi wa kutosha.

"Askari wetu watakuwa doria za miguu ambazo zitajumisha askari kanzu na askari wa kawaida pamoja na doria za magari katika kona zote za jiji la Arusha," alisema. Kuhusu upigaji wa fataki, Kamanda Masejo alisema watakaoruhusiwa ni wale tu ambao wameomba vibali na hawataruhusiwa kufyatua katika makazi ya watu na watakaokiuka maelekezo ya vibali vyao watachukuliwa hatua za kisheria.

"Katika kusherehekea Sikukuu hii ya Mwaka Mpya, ni marufuku kwa mtu au kikundi cha watu kuchoma matairi ya magari pamoja na madereva kutoendesha magari kwa mwendokasi au wakiwa wamelewa kwa sababu hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

Kamanda Masejo alisema ni marufuku kwa wazazi kwenda kwenye nyumba za vileo wakiwa na watoto wadogo huku akiwataka wamiliki wa nyumba hizo kuzingatia masharti ya leseni zao ambazo zinaonyesha muda halisi wa kufunga.

Kadhalika, aliwataka wamiliki wengine wa kumbi za starehe na maeneo mengine ya starehe kuzingatia usalama wa maeneo yao na kutojaza watu kupita kiasi.

## Bosi TEMESA ataka utendaji wenye tija

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala, amemaliza ziara fupi ya kiutendaji mkoani Dar es Salaam na kuwataka watumishi wa mkoa huo kuanza mara moja kuzifanyia kazi changamoto ambazo zinatolewa na wateja wanaotumia huduma za wakala huo.

Akiwa katika ziara ya siku mbili, Kilahala alitembelea Ofisi ya Kikosi cha Umeme Keko Darajani na kuzungumza na menejimenti ya kikosi hicho kabla ya kuzungumza na wafanyakazi.

Kilahala aliwapongeza kwa jitihada wanazozifanya na akawataka wafanyakazi hao kuhakikisha huduma wanazotoa zinaendelea kuwa bora ili kuhakikisha wanafungua fursa za maendeleo na mafanikio kwa taasisi zingine ambazo wanafanya nazo kazi.

''Niwapongeze sana, mnaonyesha mnafahamu mnachokifanya na hii ni mojawapo ya timu za TEMESA ambayo imejipanga, inafahamu inafanya nini. Kwa hiyo hongereni sana," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka watumishi hao kujitafakari na kuwa chanzo cha utatuzi wa maeneo ya changamoto wanazokumbana nazo na kutosubiri makao makuu kuja na majawabu ya changamoto hizo.

''Binafsi serikali kwa ujumla ina matumaini makubwa sana na TEMESA. TEMESA inatazamwa kama kitu kikubwa sana ina uwezo wa kufanya makubwa zaidi, ya kuwa na tija zaidi, ya kusukuma zaidi maendeleo ya nchi hii kuliko inavyofanya sasa. Kwa hiyo tunachangamoto ya kuishi mategemeo ya serikali,'' alisisitiza.

Hata hivyo, alisema TEMESA itahakikisha yale ambayo yanatekelezeka yanatekelezwa kwa mustakabali wa TEMESA na taifa kwa ujumla.

Aidha, Kilahala alipata wasaa wa kutembelea kituo cha Wakala wa Ukodishaji Magari (Government Transport Agency- GTA) katika ofisi zake zilizoko Keko Darajani na Meneja wa Kituo hicho, Mhandisi Margareth Julian, alimtembeza na akapata wasaa wa kukagua magari ya kukodisha pamoja na yadi zinazosimamiwa na kituo hicho katika maeneo ya Magomeni Usalama na Temeke.

Baada ya kutembelea kituo hicho, mtendaji mkuu alimwagiza meneja kusimamia kwa karibu mikataba ya wapangaji wa yadi zinazomilikiwa na wakala ili ufaidike na uwapo wa yadi hizo kama mali ya taasisi na kutaka kila kinachofanyika kiwe na tija na ufanisi wa hali ya juu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatutarajii kilio cha ukosefu madarasa Januari

**OKTOBA** mwaka huu serikali ilipokea mkopo wa Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19, ambazo zitaelekezwa kwenye sekta ya elimu na afya.

Rais Samia Suluhu Hassan aliweka bayana mgawanyo wa fedha hizo, wakati wa uzinduzi wa mpango wa serikali wa kuinua uchumi kwa kutumia fedha hizo.

Kwenye sekta ya elimu fedha hizo zitajenga vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari lengo likiwa ni kuwezesha wanafunzi wote kuendelea na masomo bila kikwazo.

Kwa sasa ujenzi wa vyumba vya madarasa unaendelea maeneo mbalimbali nchini, na nguvu imeelekezwa huko ili ikifika Januari kusiwe na zimamoto kama ilivyojitokeza miaka mingine na kusababisha wanafunzi kuchelewa kuingia kidato cha kwanza.

Tunaamini kila halmashauri imejipanga vyema kwa kuangalia makadirio ya miaka ya nyuma ya ufaulu wa wanafunzi na vyumba vya madarasa vinavyotakiwa, na haitarajiwi kuanza kukimbizana kubadili shule za msingi kuwa sekondari, kiasi cha miundombinu kuelemewa.

Miaka ya nyuma wananchi walijenga shule hizi kwa fedha zao na mwamko ulikuwa mkubwa kwenye baadhi ya maeneo, lakini kwingine ilikuwa ngumu kwa kuwa wananchi hawakuona umuhimu wa kuchanga.

Sasa serikali imekuja na suluhisho ni wajibu wa kamati za shule kufuatilia kwa karibu ujenzi wa miundombinu hiyo ili iwe ya kiwango, thamani ya fedha ionekane ili hata kama tutashiriki kulipa deni kama nchi tutakuwa tunafuta jasho kupitia miundombinu inayodumu.

Mara nyingi mchakato wa ununuzi husababisha gharama ya ujenzi kuwa kubwa na wakati mwingine kushangaza au thamani ya fedha kutoonekana, hivyo ni muhimu kufuatilia ili tuwe na majengo imara na sio baada ya mwaka mmoja hayafai kutumika.

Tunaamini kwa maandalizi haya sasa wanafunzi watasoma bila tatizo kwa kuwa sasa suala la miundombinu litabaki kuwa historia, kinachotakiwa ni kuboresha upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada pamoja na walimu wa kutosha.

Upatikanaji wa vitabu muhimu ni shida kwenye shule za umma ambako elimu ni bure na wazazi wengi hawana utayari wa kununua kwa ajili ya watoto wao, hivyo ni wajibu wa serikali kuhakikisha vinapatikana na wanafunzi wanafundishwa kwa kadri ya mitaala na ratiba zilizopo.

Kwenye shule nyingi za umma tatizo kubwa ni ubora wa elimu inayotolewa ambayo imebeba mambo mengi kama utayari wa walimu kufanya kazi kwa ubunifu, kujitoa na kuipenda kazi na sio kwa ajili ya kupata mshahara pekee.vLakini, wanaosimamia walimu kuhakikisha wanatoa motisha mara kwa mara kwa kuwa kazi wanayofanya ni kubwa, lakini wakati mwingine malipo ni madogo na hakuna stahiki nyingine kama ilivyo kwenye taasisi nyingine.


Kwenye shule hizi ndiko tunapata mawaziri, wakurugenzi wa taasisi mbalimbali na viongozi wengine muhimu, wote wamepikwa na mwalimu sasa ni wajibu wa kuboresha miundombinu sambamba na maslahi ya walimu, ili tusiishie kuwa na majengo mazuri, lakini bidhaa (wanafunzi) wanaotoka humo hawaendani na uwekezaji uliofanyika.

Tunaamini baada ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa sasa nguvu kubwa itakuwa ni kuboresha makazi ya walimu, ambayo ni tatizo kubwa kwa sasa kwa kuwa wengi wamejikuta wanapangiwa vituo vya kazi ila hawana pa kuishi.

Bila kuwa na walimu wenye maeneo mazuri ya kuishi na familia zao wakatuliza akili, ni ngumu kuwa na wanafunzi watakaofaulu vizuri kwa kuwa ufaulu wa wanafunzi unategemea sana kazi kubwa iliyofanywa na walimu katika kujenga ubongo wao.

Tunatarajia kuona mafanikio endelevu kwa fedha hizo ambazo ni deni litakalolipwa na Watanzania kwa miaka mingi ijayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono' kampeni ya neema kwa binti shuleni

Na Sabato Kasika

**RUSHWA** ya ngono ni miongoni mwa ukatili wa kijinsia, ambao pia ni chanzo cha athari za kiafya, kwa kuwa inaweza kusababisha maambukizi ya virusi vya Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

Ukatili huo umeendelea kuumiza jamii kimya kimya, kutokana na kwamba kitendo hicho kinafanywa kati ya watu wawili kwa siri kubwa, lakini madhara yake yanabaki kuwa ya muda mrefu kwa aliyeombwa rushwa hiyo.

Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ni miongoni mwa waathirika wa rushwa hiyo inayosababishwa na lifti za madereva wa bodaboda, bajaji na daladala, ili wawahi shule au nyumbani au wakati mwingine kupata urahisi fulani.

Wale wote wanaopitia rushwa ya ngono husababisha pia kupata mimba ambazo hazikutarajiwa na wengine huenda huwa wanatoa mimba hizo. Inaelezwa na wataalamu wa afya kuwa mara nyingi huwa si jambo salama.

Kutokana na hali hiyo, kumekuwapo kampeni mbalimbali zinazofanywa na wadau wa kupinga vitendo hivyo, ikiwamo inayoitwa 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'.

Ni kampeni inayoendeshwa na Wanawake na Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kwa kutoa elimu kuhusu rushwa hiyo kwa madereva wa bodaboda, bajaji na daladala ili waachane na vitendo hivyo.

Madereva hao wanadaiwa kushiriki katika rushwa ya ngono kwa kutumia lifti kama mtego kwa wanafunzi, hasa wale wanaotembea umbali mrefu kufuata elimu, ambao baadhi yao huangukia katika mitego ya madereva hao.

Katika kuhakikisha rushwa ya ngono inayosababishwa na lifti za madereva hao inakoma, shirika hilo limeanzisha kampeni katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke, jijini Dar es Salaam.

WAJIKI inataka wasichana na wanafunzi wa kike kwa ujumla wabaki salama wakitimiza malengo na safari yao ya maisha bila kikwazo kinachosababishwa na rushwa ya ngono.

Elimu ya kupambana na rushwa ya ngono, inahusisha madereva hao kupitia vikundi vyao chini ya udhamini wa Taasisi ya Women Tanzania Trust Fund (WTF), ambayo inaunga mkono juhudi za WAJIKI.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema shirika lake limefanikiwa kuanzisha vikundi 108 vya madereva hao vyenye wanachama 3,741 katika wilaya hizo tatu wakiwa na jukumu la kuelimisha wenzao.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, vikundi vya madereva hao ambao ni wanachama wa WAJIKI wanaelimisha wenzao ili wajue madhara ya rushwa hiyo na kuepuka kuwarubuni wanafunzi.

Binafsi ninaamini kwamba, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, hivyo ni vyema kila mmoja kuona umuhimu wa kuunga mkono kampeni ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana.'

Hatua hiyo inaweza kuleta matokeo chanya kwenye vita dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana, inayosababisha baadhi yao kutofikia malengo na hata wakati mwingine kuathiri afya zao.

Rushwa hiyo bado inaendelea kuumiza jamii kimya kimya, kwa kuwa kitendo hicho kinafanywa kati ya watu wawili kwa siri kubwa lakini madhara yake yanabaki kuwa ya muda mrefu, kwa aliyeombwa rushwa hiyo.

Cha kukumbuka ni kwamba, madereva wanapomtamani wanafunzi au wasichana kingono, hutumia nyenzo waliyo nayo wakiwasafirisha kwa malengo ya kuwalaghai na kupata rushwa tajwa ya ngono.

Hivyo, suala la mapambano dhidi ya rushwa hiyo, inawasha taa ya ukombozi kwa wasichana na wanafunzi kwa ujumla na inapaswa kupigwa vita kwa nguvu zote, ikifaa iongelewa na makundi yote, ili ikomeshwe kwa mafanikio ya kijamii.

Watu wanaotakiwa kuwapa huduma ya usafiri wanafunzi, ndiyo ambao huwaomba rushwa ya ngono na mwisho wa siku wanawaachia madhara ya kiafya. Kampeni ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono' inawezekana na iwe chachu ya mabadiliko kwetu sote.

HABARI KITAIFA

# Mapenzi walimu na wanafunzi yatikisa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Septemba 2021 walimu 931 wamefanya makosa ya utoro kazini, sawa na asilimia 51.9 ya makosa yote yaliyofanywa.

Katika kipindi hicho, walimu 105, sawa na asilimia 57.1 wameshtakiwa mahakamani kutokana na kufanya makosa hayo.

Vilevile, utovu wa nidhamu mwingine kwa walimu umeripotiwa ukihusisha vitendo vya watumishi hao kujihusisha kimapenzi na wanafunzi ambapo kwa kipindi hicho cha Julai 2020 hadi Septemba 2021, walimu 211, sawa na asilimia 11.8 wameshtakiwa.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Willy Komba, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Alisema kuwa katika makosa mazito matano ambayo yamekuwa yakijitokeza na kufanywa na walimu, kosa la utoro linaongoza.

Mwenyekiti huyo aliyataja makosa mengine kuwa ni kughushi vyeti ambapo katika kipindi cha Julai 2020-Septemba mwaka huu kulikuwa na kesi 461, sawa na asilimia 25.7 huku katika kipindi cha Julai -Septemba mwaka huu kesi za kughushi vyeti ni 41, sawa na asilimia 22.3.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha Julai-Septemba, wapo walimu waliokiuka maadili ya utumishi wa umma kwa kufanya ukaidi huku wengine wakifanya makosa ya ulevi.

"Kwa hiyo, hayo yote ni makosa mazito ambayo yanashughulikiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, lakini yapo makosa mepesi ambayo yanashughulikiwa katika ngazi ya shule," alisema Komba.

Alibainisha kuwa walimu wote waliofanya makosa hayo wamepata adhabu mbalimbali ikiwamo kufukuzwa kazi, kupewa karipio, kupunguzwa mshahara, kushushwa vyeo na wapo waliopewa onyo.

Mwenyekiti huyo aliwapongeza walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kufundisha na kulea watoto katika nyanja mbalimbali, akiwataka kuendelea kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia maadili, taratibu, miongozo na sheria zinazowaongoza.

Vilevile, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupandisha madaraja walimu wote waliostahili kupanda.

"Tangu Rais aingie madarakani, kumekuwa na neema hasa mwaka huu katika sekta ya elimu na kwa walimu baada ya kutoa kibali cha kupandisha madaraja kwa walimu wenye sifa ambapo jumla ya walimu 126,346 waliokuwa na sifa walipandishwa madaraja."alipongeza.

Kwa mujibu wa Komba, walimu waliopandishwa vyeo walirekebishiwa mishahara yao kwa wakati tofauti na hali ilivyokuwa huko nyuma.

## Atakayemwona mtoto huyo atoe taarifa

**Na Christina Mwakangale**

MKAZI wa Kawe, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, Abdallah Kondo (17), anatafutwa na familia yake baada ya kutoweka nyumbani kwao Desemba 28, mwaka huu.

Fadhili Kondo, baba mzazi wa mtoto huyo, akizungumza na Nipashe jana, alisema mwanawe alipotea maeneo ya Kimara Temboni, Mtaa wa Saranga, mkoani Dar es Salaam.

"Ni mgeni kabla hajapotea alikuwa ana siku nne Dar es Salaam tangu aje kutokea Mdaula, mkoani Pwani, kwao kabisa ni huko kwa wazazi wake.

Alikuja likizo yupo kidato cha nne, tunaomba msaada wenu kutusaidia.

"Kwa atakayemwona apige simu namba yangu ambayo ni 0716039803."

Alisema taarifa ya kupotea kwa mtoto huyo, ilitolewa Desemba 28, mwaka huu, na kupatiwa RB namba KWY/RB/2512/21 katika kituo cha Polisi Kawe.





Wananchi wakiingia kwa shida kutokana na matope yanayotiririshwa kutoka kwenye taka na kutoa harufu mbaya katika soko la Temeke Stereo, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA

## Makalla ashtukia jambo ujenzi barabara za Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameuagiza uongozi wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha unashirikiana na Baraza la Madiwani katika kuchagua barabara za kipaumbele cha ujenzi na sio kujiamulia wenyewe.

Alitoa agizo hilo wakati wa ufunguzi wa kikao cha Bodi ya Barabara, kueleza kuwa madiwani kama wawakilishi wa wananchi ndiyo wanaelewa barabara zenye uhitaji wa haraka katika kuzitengeneza, kuhitajika na wananchi wengi, hivyo ni muhimu wakashirikishwa.

Vilevile, Makalla aliwaelekeza TARURA na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuhakikisha wanalinda miundombinu ya barabara zao hususani maeneo ya waenda kwa miguu yasivamiwe tena wafanyabiashara.

Pia aliwataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya barabara kukamilisha ujenzi kwa wakati na kushirikiana na wananchi na serikali ya mtaa wa eneo husika, ili wajue nini kinaendelea katika mtaa wao.

Pamoja na hayo, Makalla aliitaka TANROADS, TARURA na makandarasi kwenda sambamba na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwafikishia wananchi maendeleo kwa wakati.

# Wanufaika TASAF watakiwa kuanzisha miradi uzalishaji

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kutumia vizuri fedha wanazopatiwa kwa kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji mali.

Ndejembi alitoa agizo hilo Mkuraga mkoani Pwani alipotembelea walengwa wa TASAF walioko katika kijiji cha Kiparang'anda A.

Alisema bila walengwa hao kutumia pesa hizo kwa kuziwekeza katika miradi midogo midogo ya uzalishaji, hawatapata maendeleo yoyote kupitia mpango huo.

Naibu Waziri alisema lengo la mpango ni kupunguza umaskini wa kaya nchini kama si kumaliza kabisa na kwamba ni vyema hilo likaendelea kusisitizwa.

"Walengwa wote wa mpango huu unaosimamiwa na TASAF, wanatakiwa watumie vizuri pesa wanazopatiwa katika kujiwekea utaratibu utakaosaidia kuinua vipato vyao kwa kuzitumia kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji. Hii itawasaidia baadaye hata kama mpango utafikia ukomo," alisema Ndejembi.

"Lengo kubwa la mpango ni kuona kaya zinasaidiwa kutoka katika hali zao za chini na kufikia kujitegemea na siyo kuona zinaendelea kubaki katika hali ile ile," aliongeza.

Pia aliwataka viongozi wa sekta mbalimbali kwenye halmashauri zote nchini na wa wilaya, kushirikiana na waratibu wa TASAF kuhakikisha kaya za walengwa zilizoko kwenye mpango zinasimamiwa kuendesha shughuli za uzalishaji na kuleta matokeo chanya.

"Nasisitiza hili la viongozi wote kushirikiana kwenye halmashauri na wilaya badala ya kuwaachia waratibu wa TASAF peke yao kwa sababu mpango huu umepelekwa kwenye kaya zilizo katika maeneo yao kwa ajili ya kupunguza umaskini wa wananchi. Kwa hiyo watumie fursa ya kuwapo mpango huu kuhakikisha wanawasimamia ili waitumie vizuri pesa hiyo wanayopatiwa kwa kuanzisha miradi midogo ya kujiongezea kipato," alisema Ndejembi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Chatherine Kisanga, alisema mpango si tu unatoa ruzuku kwa walengwa, bali pia unawajengea uwezo wa kuendesha shughuli zingine ndogo ndogo na kuanzisha vikundi vya ujasiriamali.

"Na katika kuendesha shughuli hizo pamoja na vikundi vyao, huwa tunawapelekea wataalamu wanaowapatia mafunzo ya namna ya kuziendesha kitaalamu ili wanufaike na hata wanapokopeshana kupitia vikundi vyao wanakuwa wanafahamu namna ya kutumia pesa zao.

"Kupitia mpango huu, tumeona mafanikio makubwa. Kaya nyingi kwa sasa hazipati shida tena kama ilivyokuwa awali kabla hazijaingizwa kwenye mpango. Kwa mfano suala la kukosa chakula, malazi na huduma za matibabu si tatizo tena kwao.

Kikubwa kwa sasa ni kutilia zaidi mkazo kwenye ujasiriamali na kuhakikisha wanaanzisha miradi midogo na kuisimamia vizuri ili ilete matunda," alisema.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ukarabati wa daraja la Kwasantemo lililoko Mji wa Songea Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga juzi. Daraja hilo ni kiungo muhimu katika barabara ya Gairo Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga. **PICHA: DEGE MASOLI**

# RC ataka sheria ndogo za kulinda barabara

**Na Amon Mtega,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Brigedia Jenerali, Balozi Wilbert Ibuge, ametoa wito kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani humo kuungana na halmashauri za mkoa huo kuunda sheria ndogo za matumizi ya barabara ili zisiharibiwe.

Alitoa wito huo jana alipoongoza kikao cha Bodi ya Barabara na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kisha kujadili kero mbalimbali ikiwamo uharibifu wa miundombinu unaofanywa na baadhi ya wakazi wa maeneo yaliyopitiwa na barabara hizo.

Brigedia Jenerali Ibuge, akizungumza kwenye kikao hicho ambacho kilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa mkoa huo wakiwamo baadhi ya wabunge wa majimbo ya mkoani humo, alisema kumekuwapo uharibifu wa miundombinu kwenye barabara hizo ikiwamo baadhi ya magari makubwa ya mizigo, hasa yanayobeba makaa ya mawe kumwaga mafuta au kupakia maeneo ya barabara, jambo ambalo halikubaliki kwa kuwa ni uharibifu.

Mkuu wa Mkoa alisema zikiwekwa sheria ndogo za kudhibiti uharibifu huo zitasaidia kupunguza uharibifu unaofanywa na baadhi ya watu hao ambao hawana nia njema.

Alisema Mkoa wa Ruvuma unakwenda kufungua barabara nyingi za mijini na vijijini, hivyo miundombinu yake inatakiwa kulindwa kwa nguvu zote.

Mbunge wa Songea Mjini na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, aliwataka wataalamu wa barabara kuangalia namna ya kuongeza bajeti kutokana na ukubwa wa eneo linalohitaji miundombinu mkoani humo.

Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano, aliitaka TANROADS mkoani humo kufanya upanuzi wa barabara ya Songea-Njombe kuanzia kata ya Mshangano hadi kwenye kituo cha mabasi kilichopo kata ya Shuleyatanga pamoja na kuweka taa za barabarani ili kupunguza ajali zinazotokana na msongamano.

Meneja wa TANROADS Ruvuma, Ephatar Mlavi, akipokea maagizo hayo, alisema watayafanyia kazi, ikiwamo la upanuzi wa barabara kutoka kata ya Mshangano hadi kata ya Shuleyatanga kwenye kituo cha mabasi.

# Wanaoficha wenye ulemavu waonywa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

UONGOZI wa Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, umewataka wazazi wenye watoto walio na ulemavu, kuhakikisha watoto hao wanapelekwa shuleni badala ya kuwaficha ndani.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule, alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu jitihada zinazofanywa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) unaotekelezwa na taasisi ya Foxes katika kata tatu wilayani huko kusaidia vijana na watoto wenye ulemavu kupata elimu.

Mtambule alisema taasisi hiyo imeendelea kuboresha mazingira ya elimu nchini kwa kujenga vyumba vya madarasa na shule mpya, ili watoto wote nchini wapate elimu, hivyo itashangaza kuona mzazi anamficha mtoto mwenye ulemavu na kumkoseha haki ya kupata elimu.

Alisema ni wajibu wa kila mzazi kuhakikisha mtoto mwenye umri wa kwenda shule anakwenda shule na mzazi atakayebainika amemficha mtoto mwenye ulemavu, hatua zitachukuliwa dhidi yake.

Mtambule aliwataka viongozi wa serikali ngazi ya vitongoji hadi tarafa kuhakikisha wanafuatilia taarifa za watoto wote na wale wenye sifa za kwenda shule, wapelekwe shule bila kuwatenga kwa hali waliyokuwa nayo.

Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma za Kisaikolojia Tanzania, Dk. Heriel Mfangavo, alisema mradi huo umewezesha vijana wengi kujengewa uwezo wa kisaikolojia na kiuchumi kufanya shughuli za uzalishaji na wale wanaohitaji elimu, watapatiwa elimu hasa ya ufundi kwa vijana na watoto wenye ulemavu wamepatiwa mtaalamu wa kuwachunguza aina ya ulemavu wao.

Alisema baadhi ya mambo yamekuwa chanzo cha jamii kukutwa na msongo wa mawazo kama vile kukataliwa, kutengwa na unanyapaa katika uhusiano. Pia alisema hali duni ya kiuchumi inapelekea watu kupata msongo wa mawazo, hivyo kupitia mafunzo hayo yanayotolewa, ni wazi jamii itakwenda kupunguza tatizo la msongo wa mawazo na hata kufanya shughuli kwa ufanisi zaidi.

HABARI KITAIFA

## Mkandarasi abanwa kukamilisha miradi ya miundombinu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amemwagiza mkandarasi kutoka Kampuni ya Jonta Investment, kukamilisha ujenzi wa miradi yake kwa wakati katika Manispaa ya Shinyanga.

Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, alibainisha hayo juzi wakati akikagua ujenzi wa kivuko cha watembea kwa miguu cha Upongoji Kata ya Ndala, barabara na madaraja.

Alimtaka mkandarasi huyo kuikamilisha miradi hiyo kwa wakati ili ianze kutoa huduma kwa wananchi, pamoja na kivuko hicho cha watembea kwa miguu, ambacho kitawaepusha wananchi na ajali za mara kwa mara kutokana na daraja mama kuwa finyu.

"Nakuagiza mkandarasi kama unataka kufanya kazi katika manispaa hii ya Shinyanga, miradi yako uikamilishe kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa ili idumu kwa muda mrefu kuhudumia wananchi," alisema Katambi.

Alimwagiza katika ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita sita kwa kiwango cha changarawe iliyoko Chibe Manispaa ya Shinyanga, kusawazisha vifusi pamoja na kuiwekea matoleo ya maji ili maji ya mvua yasiharibu barabara hiyo na kutengewa tena bajeti mwakani ya matengenezo.

Katika hatua nyingine, Katambi alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutafuta fedha na kuzielekeza kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya, miundombinu ya barabara na madaraja.

Kwa upande wake mkandarasi Jonh Ntalimbo, aliahidi kutii agizo la Mbunge Katambi, kuwa miradi hiyo hadi kufikia Januari mwakani itakuwa imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi, alichobakiza ni umaliziaji kwa sababu kazi kubwa ameshaimaliza. Alisema kilicho mkwamisha kukamilisha miradi ya barabara kwa wakati ni mvua kunyesha, pamoja na kuchelewa kupata vyuma vya madaraja sehemu anayoagiza.

Naye Diwani wa Ndala, Zamda Shabani, alisema kukamilika kwa kivuko cha watembea kwa miguu, kutasaidia kupunguza tatizo la ajali za mara kwa mara eneo hilo la daraja mama la Upongoji ambalo ni finyu, na kubainisha kila wiki watu kufariki kwa ajali.

# Ndejembi aonya rushwa watumishi Idara ya Ardhi

**Na Veronica Mwafisi,** MKURANGA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, ameonya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga katika kikao kazi chake na watumishi hao, Ndejembi amewataka kujirekebisha na kufanya kazi kwa uadilifu na weledi ili kuondoa migogoro inayosababishwa na utendaji kazi usioridhisha.

Alisema, watumishi wa idara hiyo wakiendelea na utamaduni wa kufanya kazi kwa kuweka maslahi binafsi mbele wataipotezea serikali mapato na kuwanyima haki wananchi wa Mkuranga kupata maendeleo yanayotokana na kodi itayokusanywa katika halmashauri hiyo.

Akisisitiza uadilifu kwa watumishi hao, Ndejembi aliwataka wabadilike kwa sababu wamekuwa wakilalamikiwa kuwaonea wananchi kwa kuwaomba rushwa na kutowashauri vizuri kwenye masuala yanayohusu umiliki wa ardhi.

"Nimeambiwa hapa Mkuranga hata mimi nikihitaji shamba natakiwa kuwa na kitu kidogo cha kuwapatia watumishi wa idara ya ardhi ambao wameweka maslahi yao binafsi mbele, na wala sitaki kumtaja mtu mmoja mmoja hapa zaidi ya kuwasisitiza mbadilike," alifafanua Ndejembi.

Kuhusu migogoro inayoibuka, Ndejembi amewataka watumishi wa idara hiyo kuwa watatuzi wa migogoro badala ya kuwa chanzo cha migogoro.

Ndejembi alifanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma wa halmashauri hiyo, ikiwa ni pamoja na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).



Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, akizungumza na wachimbaji katika eneo la Kinyambwiga lililoko Kata ya Guta wilayani Bunda mkoani Mara, alitoa agizo kwa Mkuu wa Wilaya, Ofisa Madini na Katibu Tawala wa Mkoa ambaye kwa mujibu wa kanuni ya uanzishwaji wa masoko ya madini ndiye mwenye kutafuta eneo sahihi la kuweka soko la madini, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Unyanyapaa wakosesha haki wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

UNYANYAPAA kwa watu wenye ulemavu umetajwa kuwa moja ya sababu za kuwakosesha haki zao za msingi.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi baadhi ya watu wenye ulemavu kisiwani Pemba walisema, bado jamii inayowazunguka inahitaji kupata elimu zaidi ili kuondokana na hali hiyo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya watu wenye ualbino kisiwani Pemba, Awena Khamis Rashid, alisema watu wenye ualbino wanakabiliwa na changamoto nyingi mbali na unyanyapaa, hata upatikanaji wa haki zao za msingi ikiwamo elimu na hata huduma za afya.

Alisema licha ya baadhi ya watu kuwa na uwelewa kuhusu watu hao lakini bado wanahitaji elimu zaidi kwa kuwa haijafikiwa inavyohitajika jambo ambalo linawaweka katika unyonge.

"Tunaonekana sisi wenye ulemavu kama hatuna ulazima wa kupata haki zetu za msingi jambo ambalo si halali kulifanya," alisema.

Mwenyekiti wa jumuiya ya wasioona wilaya ya mkoani, Ali Hemed Khalifa, alisema bado kuna wazazi wanaowaweka ndani watoto wao na kuwafanya kama hawana haki katika maisha yao jambo ambalo linapaswa kuchukuliwa hatua.

"Jumuiya hii inajitahidi kufuatilia wazazi wa aina hiyo na inapowagundua basi hujaribu kuwaelimisha na wapo ambao tayari wameshapata mafunzo ya ushonaji na ufumaji na wanafanyakazi hizo licha ya kuwa hawaoni," alisema.

Rabia Ali Salim wa Chakechake alisema, wenye ualbino wengi wameathirika ngozi na wengine kufanya vidonda jambo ambalo kuondoka kwake ni kupata vifaa vitakavyowasaidia na sio kuwaweka ndani.

Alisema wanaoathirika wengi wao ni watoto, kwa kuwa huwa hawajui kujilinda na kuwataka wazazi wa watoto hao wasiwadharau kwa ulemavu wao na badala wajitahidi kuwatunza ili waweze kuishi kwa usalama.

Ofisa Afya Wilaya ya Wete, Mwarabu Nuhu Mwarabu, alisema ni jambo la msingi kuhakikisha wazazi wanawasimamia watoto wao wenye ulemavu ili kujua changamoto zinazowakabili na kuwasaidia.

"Watu hawa wanahitaji uangalizi mzuri hasa wanapokuwa wadogo ili waweze kutimiza masharti yanayowafanya waweze kujiweka katika hali za usalama kwa kuwapatia huduma zao ikiwamo vigari, fimbo za kutembelea, kofia, miwani na losheni maalumu ya kuzuia jua inayolinda mionzi ya jua isiingie kwenye ngozi zao.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya watu wenye ualbino Pemba, Mudathir Sharif Khamis, alizishauri jumuiya mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali kuguswa na kuwajali watu hao kwa kuwapa fursa mbalimbali walizonazo kwa kuwapa mahitaji kama wanavyowapa wengine.

# Mbaroni tuhuma uporaji pikipiki

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuhusika na matukio ya uvunjaji na uporaji wa pikipiki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mmoja wa watuhumiwa hao aliyekuwa anasakwa kwa muda mrefu, Rashid Shaban (24), mkazi wa Mtaa wa Said Domo, Mlandizi, alikamatwa juzi Desemba 28.

Kamanda Wankyo alisema baada ya kukamatwa, mtuhumiwa huyo anadaiwa kukutwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 613 CGA nyeusi, vifaa vya kuvunjia, simu mbili, pochi ndogo za kuhifadhi fedha na vitambulisho vyenye majina ya Edward Joseph Chiwale.

Alibainisha kuwa katika mahojiano ya awali mtuhumiwa huyo aliyekuwa anatafutwa kwa muda mrefu, aliwataja wenzake watatu anaoshirikiana nao kwenye matukio ya uporaji.

Kamanda Wankyo alisema kwa sasa wako kwenye operesheni ya kuwasaka watu watano wanaodaiwa kuhusika na matukio ya utapeli kwa wafanyabiashara wa miamala ya fedha.

Alisema waathirika wa matukio matatu ya utapeli yanadaiwa kufanywa na watu hao wanaodaiwa kuingia Kibaha na kufanya wakitumia gari ndogo aina ya Sienta na kuwatishia wafanyabiashara hao kwa silaha za moto.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara hao kuchukua tahadhari kwa kufunga kamera za CCTV na kutoa taarifa kwa wakati kufanikisha watu hao kukamatwa.




Wananchi wakiingia kwa shida katika daladala kutokana na sehemu ya kituo kujaa maji katika stendi ya Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wajane watakiwa kuzingatia malezi ya watoto

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAJANE na wanaolea watoto peke yao nchini wametakiwa kutumia muda wao vizuri kwa kutenga nafasi ya malezi ili kuifanya nchi kupata viongozi wazuri kupitia watoto hao baadaye.

Wito huo ulitolewa jana na wanawake wajasiriamali kutoka asasi mbalimbali za kijamii wakati wa kongamano la wajane na wanawake wanaolea watoto wenyewe (single mothers) lililoandaliwa na Taasisi ya Usimamizi wa Mazingira UNGANISHA (UECO), liliofanyika mjini hapa.

Neema Mwakabonga alisema kuwa watoto wana vitu vizuri kwa ajili ya maisha yao ya baadaye na vinaweza kuonekana kama wataelelewa vizuri kwa kupata vyakula, elimu na malazi bora.

Aliwasihi wajane kujiepusha na imani kuwa mjane hajiwezi na ni dhaifu kwa sababu mambo hayo mara nyingi yanawakwamisha kuwa na maendeleo na malezi mazuri kwa watoto likiwamo suala la elimu na kukosa kuwa na viongozi baadaye.

Aliwataka kutumia muda mwingi kutengeneza akili zao na kwamba wanaweza kujiamini kwa kufanya biashara mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Wezesha Mabadiliko (WEMA), Dk. Lusako Mwakiluma, aliwataka wanawake hao kuhakikisha wanajenga upendo wa wao kwa wao na kutochukia wengine jambo litakalowafanya kuishi wakitegemeana katika biashara watakazoanzisha na kukuza uchumi wao.

Dk. Mwakiluma aliwaasa wanawake hao wanapoitwa kwenye makundi wasilikilie kupewa mikopo mapema bali elimu kwanza ili kujiimarisha katika kupokea na kutumia mkopo husika na kuepuka kushindwa kurejesha mikopo kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zingetatuliwa kama wangepata elimu.

Naye mmoja wa wanawake wajane waliohudhuria kongamano hilo Neema Mbasha, kutoka kikundi cha Uluguru Morogoro, aliishukuru Taasisi ya WEMA kwa kuwaimarisha kielimu mikopo na kwamba licha ya kuwa tayari wana ufugaji wa kuku 80 katika kikundi cha watu 30, wanatarajia kupata mkopo wa kuongeza na kuendesha biashara hiyo.

Naye Mkurugenzi wa (UECO), Sophia Kalinga, aliwaasa wanawake wa Manispaa ya Morogoro kuhakikisha ifikapo mwaka 2022 wawe wanamiliki uchumi wao wenyewe bila kuwa na pingamizi.

Alisema kwa kutumia majukwaa ya uchumi ya kinamama, wamejifunza mambo mengi ya kukuza uchumi na imefika wakati wajikite kwenye biashara ndogo na kubwa bila kusahau kujihusisha na upandaji wa miti ya matunda kwa ajili ya kutunza mazingira na kupata kipato kutokana na mazao yanayotokana na miti hiyo.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Profesa Felister Mombo, aliwataka wanawake hao kuujua udhaifu walionao na kuugeuza kuwa fursa katika kujiletea maendeleo.

Prof. Mombo alisema mwanamke ni mtu wa thamani katika jamii kutenda mambo mbalimbali licha ya kwamba ana nguvu, lakini ni dhaifu na akiutumia vyema udhaifu alionao anaweza kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

Zaidi ya wanawake 2000 walihudhuria kongamano hilo lililokuwa na mada mbalimbali ikiwamo, malengo, kujiamini, uchumi na uthubutu huku kaulimbiu ikiwa ni 'ujasiri wa mwanamke ni uthubutu'.

# Fisi wakwamisha mahudhurio wanafunzi shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kitongoji cha Imalange, Kata ya Sabasabini, Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, wameiangukia serikali na kuiomba kudhibiti fisi wanaotishia maisha ya wanafunzi wanaokwenda Shule ya Msingi Kabanga, iliyopo umbali wa kilometa nane.

Alisema, wanyama hao wamekuwa wakiwavizia wanafunzi nyakati za alfajiri wanapokwenda shuleni kuwahi masomo wa darasa la awali na darasa la kwanza wakilazimika kusindikizwa na wazazi wao kwa kuhofiwa kuvamiwa na wanyama hao.

Alisema kutokana na tatizo hilo, wakazi wa kitongoji hicho wamelazimika kujenga shule shikizi yenye madarasa mawili na ofisi moja ya mwalimu na kueleza kuwa mahudhurio ya wanafunzi na viwango vya elimu vinazidi kushuka kila mwaka wa masomo.

Malalamiko hayo waliyawasilisha jana katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo katika sekta ya afya, maji, barabara, kilimo na elimu.

Mmoja wa wakazi wa kitongoji hicho, Anastazia Sonda, alisema, wazazi wanapata adha ya kuwasindikiza wanafunzi shule kila siku ili kuzuia wasishambuliwe na wanyama hao wanaotoka katika pori la Hifadhi la Halmashauri ya Ushetu.

Naye Tungu Mashija alisema, wananchi waliamua kuchangishana fedha na kujenga shule shikizi yenye vyumba vya madarasa viwili na ofisi moja kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la kwanza na pili ili kuondoa adha ya wazazi kuendelea kuwasindikiza shuleni nyakati za asubuhi na kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Diwani wa Kata ya Sabasabini, Emmanuel Makashi alisema, kitongoji hicho kimezungukwa na msitu mkubwa na wanyama wakali na kuiomba serikali kupeleka walimu haraka ili kuwanusuru wanafunzi hao wakati ujenzi wa madarasa utakapokamilika.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kabanga, Charles Mussa, alisema, wanafunzi kutoka kitongoji cha Imalange, wanatembea umbali wa zaidi ya kilomita nane kufika shuleni huku wengine wakiishia njiani na kukatisha masomo yao.

Aidha, Mussa alisema, wanafunzi wanaotoka katika kitongoji hicho hawafanyi vyema katika masomo yao kwa sababu wanafika shuleni wakiwa wamechelewa na kuchoka na wakati wa mvua za masika hawahudhurii masomo kwa sababu njia wanazotumia kufika shuleni zina maji.

Kwa upande wake, Mbunge wa jimbo hilo aliahidi kutoa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa viwili na ofisi moja katika shule shikizi iliyoanzishwa na wananchi ili kuwanusuru wanafunzi kushambuliwa na fisi.

ALHAMISI DESEMBA 30, 2021

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**WAKATI CHANJO INAENDELEA... Tahadhari ya UVIKO-19, ukiukwaji wa kanuni za kinga bado ni mkubwa**



Ukurasa 12

**UNDANI AGIZO LA RAIS SAMIA...**
**Yalivyo mazito ya wanakoishi mabinti waliotelekezwa 'mimba juu ya mimba'**

# Pangani kunavyokuwa mradi wa mfano upatikanaji maji shirikishi

**Na Boniface Gideon, PANGANI**

JUMUIYA za Watumia Maji nchini ( CBWS) zilizo chini ya Wizara ya Maji, zimekuwa mkombozi katika kusaka haki ya upatikanaji maji, zikiwa chini ya Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) wilayani Pangani.

Hadi sasa CBWS ziko katika mikakati ya kuboresha miundombinu na kuhakikisha maji yanapatikana muda wote katika eneo husika, lengo ni kupunguza tatizo la kupatikana maji, hasa kwa vijiji vilivyo nje ya makao makuu ya wilaya.

Hadi sasa zimeshaanza kupiga hatua, ikiwamo kumudu ukusanyaji mapato kwa mwaka, zikiwa katika mfumo uliogawanyika katika jumuiya ndogo,

Kwakibuyu Sakura, ikiwa kinara wa ukusanyaji mapato.

Kwa mujibu wa Wakala Usambazaji Maji (RUWASA), Pangani kuna jumla ya jumuiya 20 zinazowagusa wakazi 48,382, kati ya 62,156 walioko wilayani humo.




Namna huduma ya maji ilivyo Pangani. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

**MENEJA RUWASA**

Meneja wa RUWASA Pangani, Mhandisi Rajabu Yahaya, anasema ni mtihani mgumu kwa wakala kufikia mafanikio hayo ya jumuiya ya maji, huku akikiri kuwapo msukumo mkubwa kutoka kwa waziri mwenye dhamana, ambaye pia ni mbunge wa jimbo hilo, Jumaa Aweso.

Meneja Rajabu anasema, kazi ya kusimamia Jumuiya za watumia maji ni ngumu hususani vijijini, kutokana na elimu ndogo ya jamii inayoamini maji ni huduma ya bure, hivyo wanatumia silaha ya kuunda mfumo bora wa uongozi kwenye jumuiya husika.

Anajigamba mpaka sasa kuna wingi wa jumuiya 20 zilizoko Pangani zinazotoa huduma bora za kusimamia miradi ya maji kufikia kiwango asilimia 78, ambayo ni ongezeko la asilimia tatu kutoka 75 ya wakazi.

"Ni baada ya kukamilika miradi ya Masaika, Mikocheni na tunategemea asilimia zitapanda hadi kufikia 85 utakapokamilika Mradi wa Maji wa Mbulizaga, ambao mpaka sasa unafanyiwa majaribio ya utoaji maji.

"Pia, kuna Mradi wa Maji Msaraza ambao mpaka sasa mafundi wanaendelea na kazi ya kuunganisha mfumo wa mabomba ambao tunategemea mwishoni mwa mwezi huu wa Desemba, uanze kufanya kazi," anasisitiza Mhandisi Rajabu

Anafafanua lengo lao "Ipo miradi ambayo ikikamilika, tutakuwa tumefikia lengo la asilimia 95/98 ifikapo 2023/2024, ambayo ni Mwaramshongo, Mikunguni, Mistahabu, Mekamseko, Kwakibuyu ,Mkaramo, Sakura na Mwembeni. Hii miradi ikishakamilika tutakuwa tumefikia lengo la asilimia 95/98."

**CHANGAMOTO?**

Mhandisi Rajabu anasema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni maji kuwa na chumvi nyingi, akiwa na ufafanuzi "Hili tatizo la maji kuwa na chumvi nyingi ni suala ambalo haliepukiki.

"Ni kutokana na jiografia ya eneo kubwa la wilaya hii kutawaliwa na bahari ila kinachotakiwa ni kuongeza teknolojia, hususani ya mitambo ya kusafisha na kuchuja ili kuondoa au kupunguza chumvi hii."

**WANUFAIKA MRADI**

Wananchi na viongozi wa jumuiya za watumia maji, wanaeleza furaha yao kwa kuundwa chombo hicho kinachoendana na ujio wa RUWASA.

Fatuma Zuberi, mkazi wa kata ya Masaika Godauni, anasema awali walitumia maji ya visima isiyo na usimamizi mzuri.

"Kila mtu ajichotea tu, lakini sasa hivi maji yanatoka bombani muda wote na labda kuwe hakuna umeme, lakini maji muda wote yanatoka pasipokuwa na tatizo lolote la umeme kukatika, lakini tunaomba serikali itusaidie kuondoa chumvi," anafafanua Fatuma.

Chege Salim, ni Mjumbe wa Bodi ya Maji kutoka Jumuiya ya Watumia Maji Kwakibuyu, inayoongoza katika orodha za watumia maji mkoani Tanga, kwa ukusanyaji mapato na huduma inayotoa ya maji, ikiwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya Sh. mil.300 kwa mwaka.

"Siri kubwa ya mafanikio ni kuwa na uongozi bora kuanzia Mwenyekiti wa Bodi ya Maji, Katibu wa Wajumbe na Wafanyakazi, pia tumekuwa na vikao vingi ambavyo vimekuwa msaada mkubwa hususani katika utatuzi wa changamoto zetu zinazojitokeza katika utendaji wetu wa kazi," anaeleza Salim

"Tuna Mradi mkubwa unakuja wa kuingiziwa maji majumbani, kwa hiyo kila mwananchi atakuwa habebi ndoo kichwani, bali anakuwa nayo ndani na huu mradi utakuwa faraja kubwa sana kwa wananchi, maana kilikuwa ni kilio cha muda mrefu sana cha kubeba ndoo kichwani na tunatarajia mapato yataongezeka," anasisitiza Salim

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, ambaye pia ni Diwani, Akida Baorela anakiri ni zao kubwa la mchango wa mbunge, ambaye pia ni Waziri wa Maji Jumaa Aweso, kwa kuwapa miradi mingi na kuwaletea mapinduzi makubwa ya huduma za maji.

AFYA

UNDANI AGIZO LA RAIS SAMIA...

# Yalivyo mazito ya wanakoishi mabinti waliotelekezwa 'mimba juu ya mimba'

## • Bibi afunguka undani, shule inavyowaponyoka

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa Mbeya**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni UNESCO mwaka 2000, lilipitisha kwamba 'Elimu ni Haki ya Binadamu,' sasa ikiwa ni ajenda inayochukua nafasi, ulinzi na malezi ya mtoto yanasimamiwa kitaifa hadi kimataifa, walinzi wakuu ni jamii yao.

Kisheria, mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, ikitafsiriwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto, Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, Sera ya Maendeleo ya Mtoto nchini, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Inaelekezwa, mtoto anahitaji malezi bora ili aishi vizuri, kushirikishwa kulindwa na kuendelezwa kiakili kwa ajili ya maisha yake sasa, hadi utu uzima.

**SIMULIZI YA MKASA**

Hapo ndipo ikirejewa maisha ya Hanifa (sio jina lake halisi), anapishana kwa kina na maudhui ya tafsiri hiyo, kuanzia haki ya utoto, elimu hadi malezi ya mzazi.

Amekuwa miongoni mwa wasichana waliopitia magumu, mzizi mmojawapo uko katika mimba yake masomoni, iliyomfutia ndoto zake, baada ya mama yake mzazi kufariki akiwa na umri wa miaka mitatu.

Leo, akiwa na umri wa miaka 21, anakumbuka alivyojifungua miaka mitano iliyopita yungali shuleni, sasa anaguswa mno na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, akitaka wasichana walioondoshwa masomoni kwa sababu ya mimba na nyinginezo, warejeshwe, binafsi Hanifa anatamani kuwa mnufaika.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeshatoa mwongozo ukisema waliokosa nafasi miaka miwili nyuma, ndio watakaokuwa wanufaika.

Kimsingi, kauli ya Rais Samia ambayo haina muda mrefu, inaungwa mkono kwa kiasi kikubwa na wanaharakati, pia mashirika ya kimataifa, ingawa baadhi yao wanaweka angalizo.

Ilikuwa mwaka 2015, Hanifa alipopata ujauzito masomoni kidato cha pili kwenye shule moja ya sekondari (jina tunalo) ya jijini Mbeya, baada ya kujiunga akiwa amepata fursa katika chaguo la pili, Machi 2014.

Hanifa anaielezea Nipashe akiwa kwao, Simike jijini Mbeya anakoishi na bibi yake hivi karibuni, kwamba anajutia baadhi ya mambo, wakiwamo marafiki waliomuachia funzo.

"Shule niliyokuwa nasoma umbali ni kama kilomita mbili kutoka nyumbani. Tulienda kwa miguu shuleni pamoja na rafiki zangu, niliokishi nao jirani.

"Baadhi walitumia usafiri tofauti kama vile daladala na kisha wakishuka kituo cha daladala... walitembea umbali mfupi hadi shuleni. Kwangu haikuwa rahisi kupata Sh.200 ya nauli kila siku, sina mama, baba, naishi na bibi ambaye hata mlo mmoja kwa siku ni kwa kuhangaika," anasema Hanifa.

Anasema alipoanza shule kidato cha kwanza, alinuia kufanya vizuri ili imletee mabadiliko kifamilia, kwani alikuwapo dada yake ambaye ni marehemu, naye hakufanikiwa kuendelea na masomo kutokana na mimba.

"Nilitarajia nikimaliza kidato cha nne nijiunge na kozi ya uuguzi, au hata uaskari, kwa sababu binafsi nilijua siwezi kufaulu kwa kiwango cha juu, kutokana na mazingira yangu tunayoishi.

"Nilitamani ningepata angalau cheti cha kidato cha nne ningetafuta hata kibarua, na ningeomba msaada popote kujiendeleza," anasema Hanifa.

**BAADA YA MIMBA**

Anakiri hakuwa na mahudhurio mazuri kliniki na alipojifungua anasema, aliendelea kuishi na bibi yake kwenye makazi hayo, walikosaidiwa na jamii mtaani kwao, baada ya kubaini bibi huyo hakuwa na uwezo wa kumudu upangaji.

"Baada ya miaka miwili tulitakiwa kuhama, kwa sababu mwenye nyumba ambayo tulikuwa tunakaa alikuwa anaishi nje. Aliporejea, alitutaka tuliokuwa tunaishi kwenye nyumba hiyo kuhama kupisha ukarabati.

"Kwetu ilikuwa changamoto, hatukuwa na pa kwenda. Bibi alirudi serikali ya mtaa, ndipo uongozi ukabaini ipo nyumba ambayo haijakamilika ujenzi (pagale) ingetufaa kuishi, kwa sababu mwenye nyumba aliondoka siku nyingi na hajulikani alipo.

"Tulihamia hiyo nyumba ambayo haikuwa na madirisha, tuliweka makaratasi na nailoni ili kukinga baridi, mbu na wadudu kuingia ndani na ilimpasa bibi kwenye kila mauzo awe na Sh 200 ya mafuta ya taa au mshumaa," anasimulia Hanifa.

Anasimulia wakati maisha hayo yanaendelea, dada yake waliyekuwa naye alikuwa anaumwa na hapakuwapo matibabu sahihi. Alipopata nafuu, aliamua kumuachia bibi yake mtoto wa miaka miwili, ili aende Chunya kutafuta maisha.

Anasimulia, baada ya mwaka mmoja, dada huyo alirejea akiwa mgonjwa na baada ya muda mfupi, akimuachia bibi ulezi wa kitukuu. Ni familia ambayo kwa ujumla, maisha yao ya kila siku yanategemea biashara ya mkaa inayoendeshwa na bibi huyo mlezi.

"Watoto wanakua, ikabidi waanze shule ya awali, lakini sare za shule ilikuwa changamoto. Mwanangu Junior na wa 'dadangu'(marehemu) walipata msaada kutoka kituo kimoja kinachosaidia yatima na kupata msaada, ili waanze shule.

"Ilinibidi niende kituo cha kulea watoto yatima na kutoa maelezo kwamba wazazi wa watoto hawa (wake na wa dada yake) walifariki ili kupata msaada. Yaani nami nikajiweka kundi la waliokufa. Bila hivyo, nikawaza namsaidiaje mwanangu na huyu wa dadangu? Bibi anazidi kuwa mzee, kila siku anaumwa anashinda ndani," anaeleza Hanifa.

**BIBI YAKE AFUNGUKA**

Bibi wa Hanifa, maarufu Bibi Junior (75), anaeleza alikuwa na watoto wawili, ambao malezi yao yaliegemea kwake, kwa kuwa baba wa watoto alijiengua kuwa hudumia.

"Watoto wangu walipata ujauzito hapa hapa nyumbani. Mmoja aliolewa wakatengana na mwenzake, akaamua kupanga nyumba kwingine. Kuna kipindi aliumwa sana akarudi nyumbani, alifariki," anasimulia na kuendelea:

"Hata mtoto wangu mwingine naye alifariki. Hapa nimebaki na wajukuu tu. Binti yangu aliniachia watoto (wajukuu), nao wamezaa, ninalea watoto wa wajukuu zangu."

"Hanifa alichaguliwa sekondari ya kata, niliona kama ni mwanzo wa kukombolewa, kwa sababu nimelea hawa wajukuu bila msaada wowote. Ilipofika kidato cha pili mimba, ikawa ndio basi!," anasimulia Bibi Junior na kuweka kituo cha ukimya wa takribani dakika moja, machozi yakimtoka.

Anaeleza kuwa Hanifa alipokuwa mjamzito, alipata homa za kila mara, huku akikosa pesa za matibabu, chanzo kikuu cha bajeti ya kifamilia ikiegemea biashara ya



Hanifa, akiwa katika wajihi wake wa sasa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE.**

Endelea Uk. 13

AFYA

# Yalivyo mazito ya wanakoishi mabinti waliotelekezwa 'mimba juu ya mimba'

Inatoka Uk. 12

mkaa wa rejareja, ambayo nayo ni duni maradufu.

"Kuna wakati huwa mambo yanakuwa magumu, huwa ninarudi serikali ya mtaa au kwa balozi kuomba pesa ya sukari, ili wajukuu wanywe uji. Sasa hivi ndio nina mtihani, hili pagala ninaloishi limeuzwa na mwenye nyumba, aliyenunua anataka kufungua shule ya awali, sina pa kwenda," anasema bibi Junior.

**ELIMU YA UZAZI**

Mwanasheria na Meneja Mipango wa Shirika la Wadada Solution Gender Based on Violence, Anitha Samson, anaifafanulia Nipashe kwamba, kinachochangia mimba katika umri mdogo, ni mabadiliko ya mwili kutoka utoto na kuingia kwenye balehe.

Anasema baadhi ya mabinti tangu awali hawajawahi kuambiwa kuhusu hedhi wala kuelekezwa wakiwa katika hali hiyo wanachopaswa kufanya, hivyo wanapoona mabadiliko mwilini, kama matiti na chunusi, wanapaswa kutambulishwa uhalisia na wanachopaswa kukifanya.

"Unakuta kipindi hicho wapo watoto wa kundi moja la balehe hivyo wakiona mwenzao ameota chunusi, wanamwambia ukitaka kupona fanya mapenzi. "Kumbe hata kufanya mapenzi hajui na labda yupo kwenye siku zake za hatari, hivyo hujikuta anapata mimba. Laiti angekuwa amepata taarifa sahihi kuhusiana na elimu ya afya ya uzazi mapema, pengine asingeweza kujiingiza kwenye mapenzi.

"Wengine wanaopata mimba katika umri mdogo wanakuwa wamekosa elimu ya afya ya uzazi ambayo ndani yake ina mambo mengi ya kuwasaidia watoto, hususani wa kike kuepuka mimba za mapema. Ni tofauti na mtazamo wa jamii kuwa akifundishwa ndiyo atakuwa amehamasika kujiingiza kwenye mapenzi katika umri mdogo," anaeleza.



.Wanafunzi wasichana wa shule ya sekondari iliyoko jijini Mbeya, katika tukio linalohusu elimu kwao dhidi ya mimba na hali ya jinsia yao. **PICHA: MTANDAO.**

Anitha anayejitetea anaendelea kutoa elimu hiyo kwa watoto kwa mafanikio, anataja changamoto iko kwa baadhi ya wazazi wasiofundisha watoto wao wadogo elimu ya afya ya uzazi, umri muhimu akiutaja ni kati ya miaka tisa hadi 25, akitaja eneo mojawapo ya hatari ya maradhi ya maambukizi kama Ukimwi.

Hatari ya maambukizi anataja eneo mojawapo ni janga la maambukizi ya maradhi ya Ukimwi, huku umri huo hatari kwa vijana ni kutaka kujaribu kila kitu, pasipo kujijua wako katika madhara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anarejea tamko la Umoja wa Mataifa la Mwaka 1948 kuhusu Haki za Binadamu, akitaja haki ya kila mtu kuishi na kuwa na uhuru, pia kulinda nafsi yake, hali kadhalika kupata elimu, tena akisisitiza kuwa bure hasa katika ngazi ya msingi,

Pia, Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobson, anaipongeza serikali nchini kuwarejesha masomoni wasichana waliopata mimba shule, akisisitiza haki yao ya msingi, vivyo hivyo kutomuacha nyuma mwanamke katika maendeleo.

**KUTOKA KWA MTAALAMU**

Mhadhiri Msaidizi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii cha Dar es Salaam, Zainab Rashid, anataja sababu nyingi za mabinti kupata mimba, ni zao la mabadiliko ya kimwili.

Anasema, katika malezi na ukuaji wa mtoto hasa wa kike, kila mwanajamii ana mchango wa katika uzuiaji wa mimba za utotoni.

"Familia, wazazi wafanye majukumu yao kuhahikisha watoto wanaelimishwa madhara ya kujihusisha na masuala ya uhusiano na ngono za utotoni. Watoto waelimishwe ukuaji na mabadiliko ya mwili hili lisiwe jukumu la walimu peke yao.

"Tuachane na aibu na mila zilizopitwa na wakati kwamba wazazi hawawezi kueleza watoto wao kuhusu masuala ya mahusiano na ukuaji na mabadiliko ya mwili. Pia, inapotokea msichana akapata ujauzito wamlinde na kumtia moyo na sio kumuadhibu. "Jamii pia yapaswa kubadilika hasa inapotokea msichana akapata mimba wasimuone yeye ndo mkosaji tu. Tuache unyanyapaa na kumtenga msichana huyu badala yake tumtie moyo na kumsaidia kufikia malengo yake aliyoyapanga."

Anasema pia taasisi mbalimbali kama vile zile za kidini zisiishie katika maadili ya kiimani pekee, pia ziguse elimu ya makuzi kwa vijana.

# Waendao Falme za Kiarabu waundiwa 'tenti' la Uviko Uwanja wa Ndege Dar

## • Wawekewa 'vigezo na masharti' saa 48

**Na Yasmine Protace**

MAABARA zinapokuwa na vifaa vya kisasa, inasaidia kuleta majibu bora ya vipimo na kinyume chake inazaliwa kasoro.

Ni kauli ya Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Alfello Sichwale, alipokagua mwenendo wa huduma za upimaji Uviko ndani ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Anasema hadi sasa Tanzania ina uwezo wa kupima UVIKO-19 na majibu yake yana ubora unaokubalika kikanda na dunia, kwa mujibu wa taarifa ya EAC na vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO)

Dk. Sichwale anasema maabara za Tanzania zimefanyiwa utambuzi pamoja na nchi nyingine tano za EAC, hata kukubalika mwezi uliopita.

"Maabara ya Taifa imepata asilimia 100 ya vipimo vya ubora, huku maabara nyingine za kanda zikiwa zimepata kati ya asilimia 96 na 98 za kiwango ambacho ni cha juu, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 80 kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO)," anasema.

Anasema Wizara ya Afya kupitia Maabara Kuu ya Taifa ya Jamii, imefunga mashine nyingine kubwa ya kisasa kwa ajili ya kipimo cha haraka cha Uviko -19 (PCR) kwa wasafiri wanaoenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), ikiwamo Dubai.

Anafafanua kwamba, ni baada ya UAE kutaka wasafiri wanaotoka Tanzania kwenda Dubai, wapate vipimo saa 48 kabla, kisha kumalizia saa sita kabla ya safari.

"Nimefika hapa uwanja wa ndege kujionea hali halisi na hali ni nzuri. Mashine za kutosha zipo na timu inaendelea na kazi.

"Pia, nimeshuhudia eneo la tenti nje ya uwanja ambako wateja watakapokuwa wanaanzia kupatiwa huduma. Kikubwa, wafike mapema na kwa wakati kulingana na muda wa safari zao," anasema.

Meneja wa Huduma za Afya Mipakani, pia Msimamizi Mkuu wa Huduma za Afya katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, Remidius Kakuru, anasema wizara inaendelea kupima wasafiri wanaoingia na wanaotoka nchini.

"Niwasisitize wasafiri kuwa huduma imeanza kutolewa toka tarehe 16 mwezi huu na tayari tunaendelea na upimaji wasafiri wanaoenda Dubai," anafafanua.

"Tunawasisitiza wasafiri wajitahidi wafike mapema uwanja wa ndege, ikiwezekana saa saba kabla ya safari zao na gharama hizi za kipimo cha pili ni sawa na ile ya kipimo cha kwanza," anasema.

Meneja wa Ndege (Terminal 3), Burton Komba, anafafanua: "Kwa niaba ya mamlaka ya uwanja wa ndege, tunapongeza juhudi za serikali kwa kuwezesha kuletwa mashine ndani ya siku tatu na abiria wanapatiwa huduma na sasa ndege ya Emirates itaanza kuondoka kwenda huko Dubai na tutarudi kwenye shughuli yetu kama ilivyo awali."

Katika kuhakikisha ndege hizo za kutoka Umoja wa za Falme za Kiarabu zinaendelea na safari zake nchini, meneja wa ndege hizo katika Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Julius Nyerere, Aboubakar Juma, anamhakikishia Mganga Mkuu wa Serikali, kuendelea na safari zake uwanjani hapo.

"Hapa nje tumeona tenti kubwa limefungwa na sehemu ya kuchukuliwa vipimo, tutakapokuwa tayari kutangaza kuanza kusafiri wateja wote wanaoenda Dubai, watahitajika kufika uwanja wa ndege saa saba kabla ya safari, wakiwa na 'covid test' zao za kawaida zisizo chini ya saa 48.

"Wakifika hapa watapitia eneo hili wakiwa wameshalipa 'USD 50' (Dola za marekani 50 au Sh.115,000 ) kupitia malipo ya mtandaoni ili kupunguza usumbufu hapa," anasema.

Pia, anataja taratibu zitakazotumiwa kutuma majibu yao kupitia simu zao kwa mtandao wa WhatsApp au email, kisha taratibu zingine na safari zitaendelea, akiwa na msisitizo wasafiri wanatakiwa kufanya miadi ya safari 'booking' zao kupitia mtandaoni katika muda uliopangwa na cheti kupatikana ndani ya saa 48.

Maabara Kuu ya Taifa, inatumia fursa hiyo kuwaomba wasafiri wanaotakiwa kupima uwanja wa ndege, kuwa ni ama wanaoenda au kupitia Dubai, huku wengine wakitumia utaratibu wao wa kawaida.

AFYA

WAKATI CHANJO INAENDELEA NCHINI...

# Tahadhari ya UVIKO-19, ukiukwaji wa kanuni za kinga bado ni mkubwa

## • Waziri Dk. Gwajima aanika rasmi ongezeko




Tukio la siku Tanzania ilipopokea mzigo wa kwanza wa dozi ya chanjo dhidi ya maradhi Uviko, Julai mwaka huu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

MAAMBUKIZI ya ugonjwa wa UVIKO-19 yameongezeka, huku serikali ikiendelea kuhimiza wananchi kuchukua tahadhari ambazo imewaelekeza, ili waweze kuepuka maambukizi hayo.

Idadi nyingi ya sampuli zinazopokewa katika Maabara Kuu za Taifa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anataja kuwa na sura ya kuongezeka ugonjwa huo.

Hadi sasa idadi ya sampuli zinazopokewa katika Maabara Kuu ya Taifa, zikiongezeka kutoka 14 kwa siku hadi kufikia 47, hali ikiashiria ni ongezeko la maambukizi.

Aidha, kuhusu hali ya wagonjwa wa UVIKO-19, anasema katika kila idadi ya 10, saba ni wale ambao hawajachanjwa, na wengine inatokana na kuzidiwa na magonjwa mengine kama shinikizo la damu, kisukari na Uzee.

Dk. Gwajima anafafanua hayo, alipokuwa jijini Arusha kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili, unaotekelezwa na Wizara ya Afya.

Anaonya kwamba katika wakati huu kuelekea kipindi cha Sikukuu za mwisho wa mwaka, kuna uwezekano wa maambukizi kuongezeka kutokana na watu kuendelea kushiriki shughuli zenye mikusanyiko.

Dk. Gwajima anasema wananchi wamekuwa hawachukulii suala hilo kwa uzito unaotakiwa kutokana na uhalisia wa tahadhari duni, kinyume na wanavyoelekezwa na wataalamu wa afya.

"Kasi ya kujikinga na maambukizi bado ni ndogo, licha ya kuwa wananchi wanaendelea kuchanja, bado wanahitaji msukumo," anasema Dk. Gwajima.

### HALI YA WALIOCHANJWA

Hadi kufikia Desemba 18 mwaka huu, watu zaidi ya milioni 1.2 nchini walikuwa tayari wameshapata chanjo ya kinga kamili ya kukabiliana na Uviko-19 na mikoa inayoongoza kwa kufanya vizuri katika utoaji chanjo ya ugonjwa huo ni Ruvuma, Mwanza, Dodoma, Kagera na Mara, huku mikoa ya Manyara, Njombe, Singida, Iringa na Songwe ikitajwa kufanya vibaya.

Uzinduzi wa chanjo dhidi ya ugonjwa huo, ulifanywa na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu, Ikulu jijini Dar es Salaam na kisha chanjo zikasambazwa kwenye mikoa yote nchini.

Inaelezwa, matarajio ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni kufikia asilimia 60 ya wananchi wote ambayo ni sawa na idadi ya watu milioni 35 watakaopata chanjo.

Hadi sasa kuna wastani wa kutimu miezi mitano tangu kuanza kutolewa kwa chanjo hiyo rasmi, ambapo wizara inabaini sasa kuna vikwazo vinavyosababisha idadi ya waliochanjwa kutokuwa kubwa.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof.Abel Makubi anasema taarifa potofu zilizoanza kutolewa na makundi mbalimbali ya kijamii kuhusu chanjo hiyo zimechangia kuwapo kwa hali hiyo.

"Suala la chanjo lipo nchini kwa zaidi ya miaka 100 sasa, lakini wanajitokeza baadhi ya watu wanapotosha, lakini pamoja na hayo, mwitikio wa watu kuchanja sio wa kusuasua kama ilivyo kwa nchi nyingine," Prof Makubi anasema.

Serikali nayo inaendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhakikisha upatikanaji chanjo, kuweka miongozo mbalimbali, huku Rais Samia Suluhu Hassan, akiweka mazingira bora ya wadau kuendelea kulisaidia taifa kupata chanjo nyingi zaidi.

### MWONGOZO ULIVYO

Mwongozo wa kudhibiti UVIKO-19 kupitia misongamano katika jamii, bila kuathiri shughuli za kiuchumi, toleo la kwanza unaweka wazi jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

Ni kwamba, lazima mtu avae barakoa katika vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, huku vyombo vya ulinzi na usalama vikitakiwa kusimamia utekelezaji mwongozo huo.

Pia, inaendana na angalizo penye kila kituo cha mabasi, kunapaswa kuwapo ndoo za maji tiririka ili abiria waweze kupata huduma hiyo kabla ya kupanda ndani ya vyombo hivyo vya usafiri, huku wakiwa wamevaa barakoa.

Lingine ni wananchi wanahimizwa kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, ndani ya vyombo vya usafiri kama vile daladala na mabasi ya safari ndefu, wazingatie idadi ya viti kwa kutojaza abiria kupita kiasi.

Mjumuisho wa yote unakuwa na angalizo kwamba ni mambo yanayotakiwa kufanyika, ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, lengo ni kulinda afya za abiria na wengine dhidi ya UVIKO-19, ambao bado haujapatiwa tiba

### KINACHOENDELEA

Uchunguzi wa Nipashe katika baadhi ya maeneo, umebaini kuwapo mwitikio mdogo katika uzingatiaji vigezo vya tahadhari, ikiwamo katika uvaaji barakoa.

Pia, imeshuhudiwa watu wanaendelea kukusanyika kama kawaida bila ya hatua sahihi za tahadhari kwenye vyombo vya usafiri ndani ya miji na daladala na kuna wakati wanajazana kupita kiasi, huku hata safari ndefu nako hakukushuhudiwa hatua sahihi za udhibiti.

Kwenye masoko, stendi za daladala na za mabasi yaendayo safari ndefu, bado kumeshuhudiwa msongamano mkubwa wa watu pasipo kuchukuliwa tahadhari sahihi dhidi ya ugonjwa huo hatari.

Mfano mmojawapo ni kwenye stendi ya Magufuli, jijini Dar es Salaam, ambako kuna msongamano mkubwa wa watu, hasa kwenye mageti ya kuingilia stendi hiyo, huku wengi wao wakiwa hawana barakoa.

Ni hali inayotajwa inaweza kusababisha kuenea ugonjwa huo, pale tu namna mamlaka husika hazitachukulia hatua za kuelekeza watu kuzingatia matakwa ya mwongozo wa wizara inayohusika na Afya.

Pia, ushuhuda huo wa Nipashe jijini Dar es Salaam, katika baadhi ya masoko ya Mbezi Luis na stendi ya daladala Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, kote hakuna ndoo za maji tiririka, watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida, ikikinzana na maelekezo ya kiafya ya serikali .

Ni hali inayoendelea, huku wiki hii Tanzania ikiwa imepokea tena shehena zaidi ya dozi milioni 1.6 ya chanjo dhidi ya Uviko - 19 aina ya Pfizer BioNTech kutoka Marekani, kupitia Mpango wa Kimataifa wa Usambazaji Chanjo wa Covax

Msaada huo ulipokewa rasmi na Kaimu Meneja wa Programu ya Kinga na Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Ngegwe Bulula, kutoka kwa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) nchini, Kate Somvongsiri, katika hafla fupi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Shehena ya kwanza ya dawa za namna hiyo kutoka Marekani, mwezi Julai zilipokewa zilijumuisha dozi milioni moja za aina ya Johnson and Johnson na kuiwezesha Tanzania kuzindua kampeni ya kitaifa ya chanjo dhidi ya virusi vinavyosababisha UVIKO-19.

Mwezi uliopita, serikali ya Marekani ilitoa dozi 500,000 za chanjo aina ya Pfizer BioNTech, ili kusaidia zaidi jitihada za Tanzania kukabiliana na kusambaa kwa UVIKO-19.

## Mageti kuwekwa ranchi ya Kongwa

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MENEJA wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) Kongwa, Elisa Binamungu, amesema wanakusudia kuweka mageti makubwa kwenye barabara kuu zinazopita katika ranchi kwa lengo la kulinda usalama wa hifadhi hiyo.

Pia amesema wanakusudia kuongeza mabongo yenye ujumbe wa kuwatahadharisha watumiaji wa Barabara Kuu ya Dodoma-Morogoro wanapoanza kuingia katika maeneo ya hifadhi hadi sehemu ya kutokea.

Binamungu alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe ofisini kwake wilayani hapa kuhusu kuimarisha usalama wa eneo hilo ambalo mazingira yake yamekuwa yakiharibiwa na uharibifu.

Alisema wanakusudia kuweka mageti makubwa kwenye eneo la kuingia hifadhi hiyo kwa lengo la kulinda usalama na mazingira ya eneo hilo.

Alibanisha kuwa lengo la kuweka mageti hayo ni kuhakikisha kila mtumiaji wa barabara kuu hiyo anapoingia eneo la hifadhi anapewa elimu ya utunzaji wa mazingira.

Vilevile, alisema kuwa kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Kongwa, wamekubaliana kuongeza mabango kuanzia Mji wa Kibaigwa, Mtanana na Mbande ili madereva hao kupewa tahadhari mapema kabla ya kuingia eneo la hifadhi.

Aliyataja madhara wanayopata wakati huu kwa watumiaji wa barabara hizo kuwa ni uchafuzi wa mazingira kwa kutupwa takataka mbalimbali kandokando ya barabara.

Alisema madhara mengine yanayojitokeza kwa kusababishwa na watumiaji wa barabara hiyo ni moto unaosababishwa na wavuta sigara kutupa vipisi vyenye moto.

Meneja huyo alisema kuwa kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, wataweka askari watakaokuwa na jukumu la kufanya doria usiku na mchana.

Alibainisha kuwa hifadhi hiyo ya NARCO ina ukubwa wa hekta 37,682 na inajihusisha na ufugaji wa wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Meneja huyo alisema madhara ya moto yamekuwa yakiathiri mazingira ya malisho ya wanyama hao wanaofugwa kwenye ranchi hiyo.

# Dodoma yapata mwarobaini wa uhaba mafuta ya kupikia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ILI kufikia azma ya kujitosheleza kwa mafuta ya kula, Mkoa wa Dodoma umejiwekea mkakati wa kuongeza uzalishaji wa alizeti kuanzia msimu wa kilimo 2021/22, ikiweka lengo la kulima angalau ekari 800,000 za zao hilo.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Dodoma, Benard Abraham, alibainisha hayo alipowasilisha taarifa ya idara yake kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 10 mwaka huu, takwimu zilizokusanywa na halmashauri za mkoa zilionyesha eneo lililosajiliwa kwa ajili ya kulima alizeti ni takribani ekari 583,292, sawa na asilimia 72.9 ya lengo.

"Maeneo hayo yanajumuisha mashamba ya wakulima binafsi, taasisi za elimu, mashamba ya vijiji, vyombo vya dola, vikundi vya wakulima, mashamba ya halmashauri, wafanyakazi wa serikali, ushirika wa wakulima (AMCOS), mashamba darasa ya wataalamu pamoja na wakulima wa mfano," alisema.

Aliendelea kubainisha kuwa kuna mategemeo makubwa ya eneo litakalolimwa alizeti kuongezeka kutokana na mwamko mzuri uliopo miongoni mwa wananchi pamoja na uhamasishaji, pia bei nzuri ya alizeti.

"Mkoa kwa kushirikiana na wadau ambao ni ASA (Wakala wa Mbegu wa Taifa), kampuni ya Pyxus na ZOSEM pamoja na wakulima wazalishaji wa mbegu (QDS), umefanikiwa kusambaza mbegu za alizeti kiasi cha kilogramu 280,578," alisema.

Ofisa Kilimo huyo alisema halmashuri zimeratibu uzalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa kiasi cha kilo 8,000 kwa Halmashauri ya Kongwa.

Alisema katika kuhakikisha uzalishaji wa alizeti unaongezeka, mkoa umejipanga kwa kuhusisha watu binafsi na taasisi.

"Hadi kufikia mwezi Novemba mwaka huu, jumla ya ekari 564,853 zimebainishwa kulimwa zao la alizeti kwa msimu huu wa 2021/22," alibainisha.

Alikumbusha kuwa uzinduzi rasmi wa kampeni ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta nchini ulifanywa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mwezi Juni mwaka huu mkoani Singida, ikibainishwa kwamba nchi inahitaji wastani wa tani 650,000 za mafuta ya kula.

"Upatikanaji wa mafuta hayo ndani ya nchi kwa sasa ni wastani wa tani 290,000 ambao unatokana na uzalishaji wa takriban tani 1,000,000 za alizeti, Mkoa wa Dodoma unakisiwa kuchangia tani 190,000 za alizeti, sawa na takribani tani 53,000 za mafuta ya alizeti kulingana na takwimu za uzalishaji za mwaka 2020/21," alifafanua.




Masinki ya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni yaliyoko mlango mkuu wa kuingilia soko kuu la majengo jijini Dodoma ambayo yamefadhiliwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kujilinda na ugonjwa wa corona yakionekana kutotumika kutokana na kukosa huduma ya maji na kusababisha uchakavu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Polisi yaimarisha ulinzi sherehe kuuaga mwaka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, amesema jeshi hilo mkoani humo limeimarisha ulinzi na usalama barabarani katika kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Vilevile, amewataka Watanzania kuacha kujihusisha na biashara haramu ya kubeba wahamiaji na kuwaingiza nchini kinyume cha sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Kamanda Lyanga alisema jeshi limeimarisha ulinzi na kuwataka watu kusherehekea kwa utulivu na amani.

Kuhusu usalama barabarani, Kamanda Lyanga aliwataka madereva kutumia barabara vizuri ili kuepusha ajali wakati wa sherehe hizo za kufunga na kufungua mwaka mpya.

Kamanda Lyanga pia alibainisha kuwa jeshi hilo linawashikilia wahamiaji haramu 51 raia wa Ethiopia waliokuwa wakisafirishwa kwa kutumia gari la mizigo.

Alisema askari polisi wakiwa kwenye doria barabarani, eneo la Beteko Barabara Kuu ya Dodoma-Arusha, gari lenye namba T-593 AUE, aina ya Fuso, likiendeshwa na Ignas Mgosi (33), mkazi wa Mafinga mkoani Iringa, akisaidiana na Jafari Off (39), mkazi wa Arusha, lilipekuliwa na kubainika lilikuwa na wahamiaji haramu 51 wakitokea Moshi mkoani Kilimanjaro kwenda Iringa.

"Mbinu iliyotumika ni kuwaficha chini ya matenga matupu ya nyanya na kuwafunika kwa turubai," alisema.

Kamanda Lyanga alisema Watanzania wanashiriki katika matukio ya kusafirisha wahamiaji haramu kutokana na kukosa uzalendo kwa nchi yao na tamaa ya kujipatia kipato isivyo halali kwa kuwaingiza nchini wahamiaji haramu na kuwasafirisha kwa njia haramu.

Alisema Jeshi la Polisi mkoani Dodoma linaendelea kuchunguza na kufuatilia mtandao mzima wa waliohusika na mpango huo haramu.

"Ninawaagiza wajisalimishe haraka sana kwa kuwa watakamatwa wote kokote waliko, hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa waliokamatwa zitachukuliwa, watafikishwa mahakamani kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji," alisema.

Alitoa wito kwa vijana wa Kitanzania, madereva na wamiliki wa magari kuacha kufanya vitendo vya uhalifu kwa kuwa uhalifu haulipi.

Kamanda Lyanga alisema kwa mujibu wa sheria ya nchi, siyo tu watuhumiwa kufikishwa mahakamani na kupata hukumu ya kifungo bali pia gari lililohusika hutaifishwa. Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji, Adam Mkuyu, alisema majeshi yanafanya kazi kwa ushirikiano na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano.

Alisema wageni wanatakiwa kuingia nchini kwa kufuata sheria na utaratibu, vinginevyo ni kuvunja sheria za nchi.

"Wananchi watoe taarifa pindi wanapoona kuna wahamiaji haramu, hapa Dodoma kila kata ina Ofisa Uhamiaji wa Kata," alisema.



# ‘Miradi iendane na thamani ya fedha’

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa halmashauri zote mkoani Mbeya wameagizwa kuwasimamia makandarasi na mafundi wanaotekeleza miradi ya serikali ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyoendana na fedha zinazotolewa.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya ilipokua inakagua utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba 92 vya madarasa katika shule mbalimbali za sekondari katika Jiji la Mbeya.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema katika shule sita walizotembelea waliridhika na ujenzi wa vyumba hivyo pamoja na miundombinu mingine na kwamba miradi imetekelezwa vizuri kwa sababu ya usimamizi mzuri.

Alisema miradi yote inaonekana imetekelezwa na mafundi wa mitaani, lakini ina ubora mkubwa ambao unaendana na fedha ambazo zilitolewa na serikali, hivyo akawataka viongozi kutumia mfumo huo kusimamia miradi mingine.

Mwakasole alisema miradi mingi imetekelezwa kwa uaminifu na imekamilika ndani ya muda uliopangwa na serikali na kuna uwezekano mkubwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani wakaanza kwa wakati.

“Tunashukuru miradi hii imetekelezwa na mafundi wetu wa mitaani ambao kwa muda mrefu tulikuwa tunawaona wanaunga tu viraka mitaani, sasa kila mradi tunaoutembelea tunakuta umejengwa kwa viwango, vyumba vyote utadhani vimejengwa na fundi mmoja,” alisema Mwakasole.

Alisema kamati hiyo itaendelea kuisimamia serikali ili kuhakikisha kodi za wananchi zinatumika vizuri katika kila sekta ambayo inapatiwa miradi ya kutekeleza.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, alisema halmashauri hiyo ilipatiwa Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule za sekondari 29 zilizoko jijini humo.

Alisema katika shule hizo walikuwa wanajenga vyumba 92 ambavyo kwa kiasi kikubwa vimekamilika na viko tayari kupokea wanafunzi mwezi Januari na vimekamilika kutokana na usimamizi mzuri wa viongozi wa jiji hilo.

Dk. Tulia ambaye ni Naibu Spika aliwaomba wajumbe wa Kamati ya Siasa kukagua miradi hiyo kwa kuwa alisema wakati mwingine ukaguzi huo unasaidia utendaji wa viongozi hao kuwa mzuri.

Aliwaomba waendelee kukagua miradi mingine ambayo inatekelezwa kwa kutumia fedha zinazotoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwamo inayotekelezwa kwa nguvu za wananchi, halmashauri na Serikali Kuu.

“Leo mmetembelea shule sita ambazo zinawakilisha shule zingine 23 zilizobaki, tunawahakikishia kwamba viwango mlivyoviona kwenye shule hizi ndio hivyo hivyo na kwenye shule zingine, lakini tunawaomba mwendelee kukagua na miradi mingine,” alisema Dk. Tulia.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, Oliver Kibona, aliwataka viongozi wa halmashauri kujenga miradi kwa kuzingatia watu wa makundi yote wakiwamo wenye ulemavu.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole (aliyeshika kipaza sauti), akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya chama hicho pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya baada ya kukamilisha ukaguzi wa miradi ya elimu juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mpango shirikishi waongeza idadi chanjo UVIKO-19

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

MPANGO harakishi na shirikishi kwa jamii wa kuhamasisha kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 umeongeza idadi ya wananchi wanaojitokeza kupata chanjo katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe kutoka watu watano kwa siku hadi 40.

Mkoa wa Songwe ulikuwa miongoni mwa mitano ya mwisho nchini kwa wananchi wake kutojitokeza kupata chanjo hiyo, hali iliyoilazimu serikali kuuingiza kwenye kundi la mikoa ya kuwekewa mkazo hasa kutumia mpango shirikishi na harakishi.

Akizungumza wakati wa kuanza utekelezaji wa Mpango huo awamu ya pili mkoani Songwe, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Dk. Enock Mwambalaswa, alisema kabla ya mpango huo wananchi walikuwa hawajitokezi kupata chanjo.

Alisema kwa siku walikuwa wanapokea kati ya mtu mmoja na watano wanaotaka chanjo na siku zingine zilikuwa zinapita bila kuchanja mtu jambo lililokuwa linawakatisha tamaa wahamasishaji.

Alisema baada ya kuanza kutekelezwa kwa mpango huo, wananchi wameanza kuongezeka kwa kiwango kikubwa hali ambayo wakati mwingine inawafanya wachanjaji kuelemewa na idadi kubwa ya watu wanaojitokeza.

“Kwa sasa tukipokea watu wachache huwa wanakuwa 30, lakini wakati mwingine wanazidi 40, tunaamini kwamba ile elimu ambayo tuliwapatia viongozi wa ngazi ya jamii bado inafanya kazi na ndiyo maana idadi ya wanaojitokeza inaongezeka,” alisema Dk. Mwambalaswa.

Alisema sasa hivi kazi ya uhamasishaji sio ngumu kwa sababu wanasaidiwa na viongozi wa serikali za mitaa ambao wana uelewa mkubwa na wao wanashiriki kwenye uhamasishaji.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Family Care cha mjini Tunduma, Aliko Mbembela, alisema kwa sasa kazi kubwa waliyonayo ni kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema walianza kuwahamasisha watumishi wa umma ambao kwa sasa pia wanashiriki kwenye uhamasishaji wa jamii na kwamba wao ndiyo walioanza kuchanjwa ili kuwa mfano kwa wale wanaowahamasisha.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Dk. Mponjili Mwangozi, alisema ili kufanikisha zoezi hilo wamegawa timu za watu mbalimbali ambao wanashiriki kwenye uhamasishaji.

Alisema wilaya hiyo ina vijiji na mitaa 127 ambayo imegawanywa na wanashirikiana na watoa huduma ngazi ya jamii kwenye uhamasishaji wa wananchi.

Kiongozi wa timu ya uhamasishaji wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 kutoka katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Subisya Kabuje, alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe kujitokeza kuchanjwa ili wajikinge wao na watu wengine.

Alisema chanjo zote zinazotumika nchini zimethibitishwa na wataalamu kwamba ni salama na hazina madhara ya aina yoyote.

Alisema mtu akipata chanjo hiyo anaendelea na majukumu yake kama kawaida na kuwataka wananchi kuacha kusikiliza maneno ya mitaani badala yake wawasikilize wataalamu.

## Walitaka Jiji kuondoa taka zinazohatarisha afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Itiji katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameuomba uongozi wa jiji hilo kuondoa haraka maghuba ya taka ambazo zikikaa muda mrefu bila kuondolewa zinatoa harufu na kuwa kero.

Walisema taka hizo zinahatarisha afya za baadhi ya watoto wanaocheza kwenye maghuba hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Gideon Mwatebela, alisema maghuba hayo yamekuwa yakiwasaidia kutunza taka lakini yanapokaa muda mrefu yanageuka kero.

Alisema taka huwa zinasambazwa na upepo mpaka kwenye makazi ya wananchi na kusababisha kero kwao na baadhi ya watu ambao wanasaka baadhi ya vitu ikiwamo chupa za plastiki kwa ajili ya kuuza ambao huwa wanashiriki pia kusambaza taka hizo.

“Kama unavyoona hili eneo watoto wote wanacheza hapa, wengine wanaokota hayo makaratasi kwa ajili ya kutengeneza mipira hali ambayo inahatarisha maisha yao, lakini zikioza zinatoa harufu mbaya sana,” alisema Mwatebela.

Naye Amina Shomary, alisema wananchi wanatoa fedha kila mwezi kwa ajili ya kuzoa taka, lakini wanashangaa taka hizo kukaa muda mrefu bila kuondolewa.

Halmashauri ya Jiji la Mbeya ni miongoni mwa miji iliyopatiwa msaada wa magari na maghuba ya kuzolea taka, lakini uondoshaji wa taka hizo umekuwa tatizo.



# 350 kushiriki tamasha la maonyesho ya biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAMASHA la maonyesho ya nane ya biashara linatarajiwa kufunguliwa kufanyika Januari 2, mwakani kwa kuwashirikisha wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali kutoka nje na ndani ya nchi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo, Waziri wa Biashara, Maendeleo na Viwanda, Omar Said Shabani, alisema teknolojia na ubunifu katika ukuaji wa biashara ni muhimu kuhamasisha matumizi yake na ubunifu ili kuchochea biashara.

"Dunia ya sasa ipo katika mapinduzi ya nne ya biashara na teknolojia imechukua nafasi yake ambapo biashara zimekua zikitumika mitandaoni kutokana na UVIKO-19," alisema.

Alisema lengo la wizara yake ni kuona teknolojia na ubunifu inakuwa sehemu kubwa ya ufanyaji wa biashara iwe kutafuta masoko na mauzo.

Alisema kuwa maonyesho hayo yatatoa fursa kwa wafanyabiashara na wazalishaji kutoka ndani na nje ya Zanzibar kuonyesha bidhaa zao na huduma zao ili wananchi wazifahamu na kujua mahitaji yao.

Alisema tamasha hilo litakuwa na washiriki 350 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika ikiwamo Misri, Uganda, Burundi, Kenya, Tanzania Bara na wenyeji wao Zanzibar.

Alisema idadi ya washiriki kwa mwaka huu imeongezeka ikilinganishwa na maonyesho ya mwaka jana ambayo yalikuwa na washiriki 325.

"Washiriki wa maonyesho hayo wapo wajasiriamali wadogo, wazalishaji wa viwanda, taasisi za serikali zinazotoa huduma mbalimbali," alisema.

Alisema katika tamasha hilo kutakuwa na siku maalum kwa lengo la kuongeza uelewa kwa watu, kutakuwa na siku maalumu ya ubunifu ili kuwahamasisha wabunifu wachanga na wakongwe kazi zao zitambulike na kuongeza thamani katika uchumi.

Tamasha hilo litakalofanyika katika viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar ni miongoni mwa shamrashamra za sherehe za miaka 58 ya Mapinduzi na linatarajiwa kufunguliwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud na litafungwa Januari 15.

## Wawekezaji sekta ya kilimo wakaribishwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakaribisha wawekezaji watakaowekeza katika sekta ya kilimo ikiwamo mazao ya viungo kuwezesha wakulima kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya mapinduzi katika sekta hiyo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudriki Ramadhan Soraga, wakati alipofanya mazungumzo na mwekezaji kutoka Brazil akifuatana na balozi wa heshima wa nchi hiyo aliyekuwapo Zanzibar, Abdulswamadu Abdulrahim, ofisini kwake Mwanakwerekwe.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejikita kuona sekta ya kilimo inakuwa mkombozi na kuleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wakulima kwa kulima kisasa na kwa tija.

Alisema kilimo cha viungo ikiwamo vanila bei yake katika soko la kimataifa ni kubwa ambayo inaweza kubadilisha maisha ya wakulima kuwa bora na kujitegemea.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumejikita katika kuimarisha sekta ya kilimo ikiwamo cha viungo na tayari ipo miradi mbalimbali inayotekelezwa na asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa ikiwamo mradi wa mazao ya viungo," alisema.

Naye Balozi Abdulrahim alisema wapo wawekezaji waliotia nia ya kuwekeza katika sekta ya kilimo cha viungo biashara hatua ambayo itasaidia kuleta mabadiliko katika sekta hiyo.

Alisema mazingira ya kisiwa cha Zanzibar pamoja na jiografia yake ni nzuri yenye kutoa nafasi kubwa ya maendeleo ya sekta ya kilimo cha viungo cha biashara na kubadilisha maisha ya wakulima kuwa bora.

Alisema vanila iliyolimwa katika baadhi ya maeneo ya kisiwa cha Pemba ni yenye ubora wa hali ya juu sawa na inayolimwa katika nchi ya kisiwa cha Comoro ambayo inaongoza duniani kwa kilimo hicho.

"Wawekezaji kutoka Brazil wameonyesha nia ya dhati ya kuwekeza katika sekta ya kilimo cha mazao ya viungo ikiwamo vanila ambacho kwa sasa bei yake katika soko la dunia ni kubwa yenye kuleta matumaini makubwa," alisema.

**Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudriki Ramadhan Soraga, wakati alipofanya mazungumzo na mwekezaji kutoka Brazil akifuatana na balozi wa heshima wa nchi hiyo aliyekuwapo Zanzibar, Abdulswamadu Abdulrahim, ofisini kwake Mwanakwerekwe.**




Watalii kutoka Ufaransa wakipanda boti kwenye Bandari ya Zanzibar kuelekea kisiwa kidogo cha Changu kuangalia kobe, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Kiongozi KMKM ahamasisha askari kuchanja UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Komodoo Azan Hassan Msingiri, amesema ingawa kupata chanjo ya UVIKO- 19 ni hiari, lakini idadi ya maofisa na askari wa kikosi hicho waliochanja hairidhishi.

Aliwataka maofisa na wapiganaji wa kikosi hicho kuchanja ili kujikinga na ugonjwa huo.

Hayo aliyasema jana Makao Makuu ya KMKM Kibweni, wakati akizungumza na askari hao katika mkutano maalumu wa kufunga mwaka 2021. Alisema maradhi hayo yapo na sasa ni wimbi la nne limekuja kwa mtindo mwingine na kutumia mkutano huo kuwashauri wapiganaji na maofisa kuacha imani potofu hasa wasiowatakia mema wananchi wa Zanzibar na Tanzania.

Alisema ni jambo la ajabu kuona askari wa KMKM hajachanja chanjo hiyo kwasababu Hospitali ya KMKM inatoa huduma hiyo ambayo inafuatwa na watu kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar. "Ingawa ni hiari kuchanja chanjo ya corona, lakini siridhishwi kabisa kuona askari anapata maambukizi ya maradhi hayo hatari huku akigundulika kuwa hajapata chanjo," alisema.

Akizungumzia maendeleo ya mwaka mmoja kikosi hicho ni kujitegemea kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uvuvi wa bahari kuu ambao ulianza kwa majaribio Agosti 16, mwaka huu, kwa meli ya uvuvi ambayo kikosi cha KMKM kiliingia ubia na Kampuni ya Tijara Marine Services.

Alisema katika shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi wanatarajia kufungua uvuvi wa bahari kuu huko Makao Makuu ya KMKM Kibweni na uzinduzi wa mradi wa kiwanda cha kutengeneza mikate ya boflo.

Komodoo Msingiri alisema katika kipindi hicho kifupi cha uongozi wake akiwa Mkuu wa KMKM ameleta wawekezaji mbalimbali katika kikosi mfano mfanyabiashara Mohamed Dewji ambaye amekuwa akitoa huduma kusambaza chakula kikosini hapo.

Alisema mwekezaji mwingine aliyefika kikosini hapo ni Mohammed Mbaye kutoka katika Kampuni ya Oil Com ya Tanzania Bara ambaye ana mpango wa kuwekeza katika ufugaji wa samaki na kiwanda cha kukobolea sembe.

Naye Kaimu Mkuu wa Utawala na fedha wa kikosi hicho, Kamanda Juma Saleh Seif, amewataka askari wa KMKM kufanyakazi kwa bidii na kuisaidia nchi kupata maendeleo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU NAMBA**: **0745 222 312 / 0715 768 811.**

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUKURU JKT KIWANJA KIPO KISUKURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

## NAFASI ZA UALIMU

NAFASI ZA KAZI YA UALIMU DIPLOMA AU DIGRII YA KIINGEREZA,HESABU NA SCIENCE CHEKECHEA NA DARASA LA 6 NA 7 **SIMU: 0783298900**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRENK DEUS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3038/0020** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **NYAKURUNDUMA** mwaka **2014**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **KAT/MPA/RB/503012/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABEID MANYANDA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0938-0053** kilichotolewa na baraza kupitia shule ya secondary ya **MBEZI BEACH mwaka 2002** na cheti cha kidato cha sita index namba S0731-0630 kilichotolewa na baraza kupitia shule ya secondary ya **MAKONGO mwaka 2005** na cheti cha chuo cha **THE SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA** kozi ya **BACHELOR OF BUSINESS ADMINISTRATION** registration No. BBA 1920 kilichotolewa mwaka 2008, Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/568182/2021**

## KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 28/01/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA TOYOTA WISH T 124 DHP, MALI YA ALPHA FILIMON MATANDO BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, P.O. BOX 4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWANAISHA HAMISI SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CAMI** yenye namba za usajili **T 593 BKM** chasis namba **J122E00690**, engine namba **K300824361**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

DAR/MBU/RB/607065/2021

## REALITY MANUFACTURING LIMITED

**MINUTES OF THE EMERGENCY MEETING HELD AT COMPANYS OFFOCE AT TABATA KIMANGA, LIWITI WARD, NEAR MAZDA RECREATIONS CENTER ON 15TH OCTOBER, 2021 AT 16.00PM**

**PRESENT:** Jeff Micah Shellembi - Member . chairperson Berina Kahabi Mhuli – Member/Acting Secretary Neema Jeff Shellembi – Member

**MINUTE 1/022: QUORUM**
With the necessary quorum in place, the Chairperson declared the meeting properly convened and constituted.

**MINUTE3/022 MINUTES**
As this was the emergency meeting there was no previous Minutes to be signed by the chairperson.

**MINUTE 3/022 VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY.**
That company has since its formation not managed to operate as thus being operated at loss.
**RESOLVED:** That the meeting proposed and approved that by this special resolution it is agreed that it be wound up voluntarily.
There being no other business to transact, the meeting was closed at 17:00pm.

## IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO

**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 75 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late ALEX MGWELELE MWASILE**

**By 1. MGWELELE ALEX MWASILE**
**2. ………………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 11 day of JAN.. 2022
**Dated at MOROGORO this 28 day of DEC………2021**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MICHAEL SANGATI EMMANUEL**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj aina ya **TVS KING** yenye namba za usajili **MC 674 BML** Chassis No. MD6M14PK8G4F24007 Engine No. 0K4FG4036435 Yenye rangi RED Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.
Taarifa ya Polisi: MWA/NY/RB/593114/2021

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Bintiye Tutu akumbuka baba yake akimwokoa kijana kuchomwa moto

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI



Nontombi Tutu, akizungumza nyumbani kwao mjini Cape Town, nchini Afrika Kusini. **PICHA: TimesLIVE**

WAKATI dunia ikiendelea kuyaeleza na kusherehekea maisha ambayo aliyaishi Askofu Desmond Tutu, kwenye jamii kwa kuonyesha upendo kwa waliokumbwa na dhuluma, unyanyasaji, bintiye anamuelezea baba yake, akisema akiwa nyumbani alitenda hayo pia.

Waafrika Kusini, wanamkumbuka mshindi huyo wa Tuzo ya Nobel, mwaka 1984, kutokana na harakati katika kupinga ubaguzi wa rangi, huku binti yake akisimulia ambavyo alimshuhudia baba yake, akimuokoa kijana aliyeponea chupuchupu kufa kwa kuchomwa moto.

Nontombi Naomi Tutu (61), anasema kifo cha baba yake kilichotokea mwishoni mwa wiki, kinamkumbusha matukio mengi yanayomfanya ajivunie maisha ya mzazi wake, ikiwamo upendo huku akimuokoa kijana mmoja kuuawa kwa kuchomwa moto na kundi la watu wenye hasira.

Anasema mwaka 1985, nchi ikiwa katika harakati za ukombozi huku chama tawala cha African National Congress (ANC), kikijaribu kukabiliana na shinikizo la kisiasa na kuupindua utawala wa wazungu wachache yalitokea matukio kadhaa ikiwamo mapigano hata vifo.

"Katika mazishi ilikuwa Julai (1985) maeneo ya Johannesburg, kanda za video zilizohifadhiwa zinaonyesha Tutu (baba yake), waziwazi akiwa na mavazi ya zambarau ya ukasisi, akiingia kwa nyuma kusukuma kundi la waombolezaji na vijana wenye hasira ambao walikuwa wakimpiga kwa mateke mwanamume asiye na ulinzi, ambaye alionekana kujikunja chini katika vumbi.

Akishutumiwa kuwa ni mshirika wa ubaguzi wa rangi, akamwagiwa petroli na alifungwa pingu, walisema tunaweka tairi shingoni mwako, na kisha kuwashwa moto. Tutu aliingilia kati pamoja na makasisi wengine, ili kumuokoa kijana.

"Nilipomuona kwenye kanda hiyo akifanya hivyo, nilishangazwa, yalikuwapo mengi ya kushangaza," anasimulia jana, Nontombi, mmoja kati ya watoto wanne wa Askofu Tutu, wakati akizungumza na shirika la habari la Reuters, nyumbani kwao, Cape Town.

"Tutu alihubiri na aliusema utawala dhalimu wa watu weupe walio wachache nchini Afrika Kusini, ambao ulifikia kikomo katika miaka ya 1990, na alizungumza mara kwa mara kwenye mazishi ya wanaharakati vijana waliouawa na vyombo vya usalama vya serikali."

Nontombi, ni mchungaji, anafanana sana na baba yake katika maisha, anakumbuka safari walizozifanya familia kutoka Alice huko Eastern Cape hadi Swaziland (Eswatini), akiwa na ndugu zake watatu, kuelekea shuleni.

"Alikuwa ni baba wa kawaida. Alipenda kukumbatia. Jambo moja ninalopaswa kusema, alikuwa na nidhamu, kuna wakati baba alisema: Nimekatishwa tamaa'. Mara nyingi, ujue lilikuwa gumu sana na hilo ndilo ambalo hatukuwahi kulitaka, kumkatisha tamaa baba, ilikuwa si rahisi kumkatisha tamaa, ilichukua muda mwingi kumkatisha tamaa," anasema Nontombi.

Jana, Wakfu wa Desmond & Leah Tutu ulitoa taarifa kwamba, ili kuwapa nafasi waombolezaji wanaotaka kuzuru Kanisa Kuu la St George na kutoa heshima zao za mwisho, Tutu, alihifadhiwa katika kanisa hilo hadi Ijumaa, kutoa nafasi kwa waombolezaji.

Askofu Tutu, ambaye hakutaka matumizi makubwa na ya kifahari, aliomba jeneza lake liwe la bei nafuu sana, litakalochomwa kwa faragha na majivu yake kuzikwa katika kanisa hilo, wakfu huo ulisema.

**RAMBIRAMBI**

Viongozi kutoka kote duniani wametoa risala zao, akiwamo rais Biden akisema "alivunjika moyo kufahamu kuhusu kufariki kwa mtumishi wa kweli wa Mungu na wa watu, akisema : urithi wa Tutu unavuka mipaka na utaendelea kwa muda mrefu.

Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama, alimtaja Tutu kama mshauri, rafiki na dira ya maadili, huku Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Gutteres pia akitoa salamu za rambirambi.

Kadhalika, ujumbe wa Malkia Elizabeth II wa Uingereza, ulisema, anamkumbuka Tutu, kwa furaha wakiwa katika mikutano pamoja naye na ucheshi.

"Kuaga dunia kwa Askofu Mkuu Tutu kutahisiwa na watu wa Afrika Kusini na watu wengi huko Uingereza, Ireland ya Kaskazini na katika Jumuiya ya Madola, ambapo alishikiliwa kwa upendo na heshima kubwa."

Vatican, ilisema katika taarifa kwamba Papa Francis alitoa rambirambi za moyoni kwa familia yake na wapendwa wake.

"Kupigania uhuru kutoka kwenye mahandaki kuitetea Afrika Kusini, kulihitaji ujasiri ambao hauwezi kuelezeka," Graca Machel, mjane wa Nelson Mandela, alisema katika taarifa yake.



**ALIYOTENDA**

Alijulikana kwa upendo kama The Arch, Tutu alitambulika papo hapo, akiwa na mavazi yake ya zambarau ya ukasisi, hali ya uchangamfu na tabasamu karibu kila mara, alionyesha hisia zake hadharani, licha ya umaarufu wake, hakuwa mtu ambaye alipendwa na wote.

Alitawazwa kama kuhani mwaka wa 1960, na aliendelea kuhudumu kama Askofu wa Lesotho kuanzia 1976 hadi 1978, Askofu Msaidizi wa Johannesburg na Mkuu wa Parokia, Soweto.

Alikuwa Askofu wa Johannesburg mwaka 1985 na aliteuliwa kuwa Askofu Mkuu wa kwanza mweusi wa Cape Town mwaka uliofuata.

Baada ya Mandela kuwa rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini mwaka 1994, Tutu aliteuliwa naye kwenye Tume ya Ukweli na Maridhiano iliyoundwa kuchunguza uhalifu uliofanywa na wazungu na weusi wakati wa enzi ya ubaguzi wa rangi.

**MAZISHI**

Askofu Tutu, leo, Ijumaa, atalala katika Kanisa Kuu la St George, kabla ya ibada ya mazishi keshokutwa, itakayoongozwa na Askofu Mkuu Makgoba.

"Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa watu na mashirika kote nchini na duniani kote kwa kumiminiwa upendo, heshima na rambirambi kufuatia kifo cha Askofu," Askofu Mkuu Tutu IP Trust na Wakfu wa urithi wa Desmond & Leah Tutu walisema katika taarifa yao.

**Makala hii imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa Mtandao.**

HABARI MICHEZO

# SIMBA: HATUDHARAU NA HATUOGOPI YEYOTE CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa haitoiogopa wala kuidharau timu yoyote ile kwenye mechi za makundi ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika itakayoanza kutimua vumbi kuanzia Februari 11, mwakani.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema wamepokea kwa mikono miwili droo iliyochezeshwa juzi Cairo nchini Misri, hivyo wanachofanya ni kujipanga kucheza si na timu hizo tu ambazo wako nazo pamoja kwenye kundi, lakini timu yoyote ile ambayo watacheza nayo baada ya hapo.

Simba imepangwa kwenye Kundi D la michuano hiyo, ikiwa pamoja na timu za Asec Mimosas ya Ivory Coast, RS Berkane ya Morocco na USGN ya Niger.

"Tumepokea kwa mikono miwili droo iliyochezeshwa, sisi kama Simba timu yetu ni ya kucheza mpira na si kuanza kuangalia kundi gumu au jepesi, sisi yeyote yule ambaye tungepangiwa naye tungecheza. Baada ya droo hiyo sasa kama uongozi tunajipanga kwa ajili ya maandalizi, timu yetu iko vizuri, na tutafanya marekebisho, Simba haijawahi kuogopa timu yoyote ile, tumeshacheza na timu nyingi kubwa barani Afrika na hata Ulaya, lakini hatuzidharau timu tulizopangwa nazo, tutapambana," alisema Mangungu.

Simba itaanzia nyumbani kwenye mechi hizo za makundi dhidi ya Asec Mimosas, timu ambayo ilicheza nayo mara mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi mwaka 2003 mara ya kwanza ilikuwa Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Agosti 24 mwaka huo, Simba ikishinda bao 1-0 lililofungwa na Ulimboka Mwakingwe, na mechi iliyochezwa nchini Ivory Coast, Oktoba 19, Simba ilikubali kichapo cha mabao 4-3 na kushindwa kusonga mbele kwenye hatua ya robo fainali baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye Kundi A.

BONASI...




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Nelson Minyeri Lusingu, kutoka Kanyigo, Kagera akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 27.2 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# Namungo kusajili mabeki wawili

**Na Saada Akida**

HUKU ikielezwa kwamba imelenga kuimarisha kikosi chao kwa kumulika nafasi mbili kwenye dirisha hili dogo linalotarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani, uongozi wa Namungo FC umesema tayari umempata kocha mkuu kutoka Zambia na muda wowote utamtangaza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Selemani, alisema kumekuwa na tatizo katika nafasi mbili; beki wa kulia na kati baada ya Haruna Shamte kupata majeraha na kukaa nje kwa muda mrefu.

Alisema baada ya kuumia kwa Haruna wamebaki na beki wa kulia mmoja hali inayowalazimu kutafuta watu ambao watakuja kusaidiana naye.

"Ripoti tuliyopewa imeeleza juu ya nafasi ya ulinzi, kulingana na tulivyoona timu katika mechi hizi 10, tumeona kwamba tunahitaji kufanyia kazi nafasi hiyo ya ulinzi hasa beki ya kulia ambayo kwa sasa amebaki mchezaji mmoja baada ya Haruna kuumia na kutakiwa kukaa nje wiki tatu," alisema katibu huyo.

Alisema wanaangalia usajili wao ndani na nje ya nchini, pia wanahitaji kuwapata mapema nyota hao ili kwenda kuwafanyia majaribio katika michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar.

Katibu huyo alisema baada kumtambulisha kocha wa makipa, Josia Steven, muda wowote kuanzia sasa watamtangaza kocha mkuu na kwamba tayari yuko mkoani Lindi kwa ajili ya kurithi mikoba ya Hemed Morocco.

"Ni kweli tumempata mrithi wa kocha Morocco, anatoka nchini Zambia (jina ni mapema sana), lakini kuanzia sasa tutamtambulisha,"alisema Ally.

## Kisiwani yaongoza kugawa pointi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Ligi Kuu Zanzibar ikisimama kupisha michuano ya Kombe la Mpinduzi timu ya Kisiwani imefunga mzunguko huo wa kwanza kwa kuburuza mkia katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, huku KMKM ikiendelea kutesa kileleni.

Katika michezo 15, Kisiwani imepoteza mechi 13 na kushinda miwili tu, huku ikifuatiwa na Machomane ambayo imefungwa mechi 10, ikashinda miwili na sare tatu.

Akizungumza na gazeti hili juzi visiwani hapa, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Haji Issa Kidali, alisema wanatarajia kukutana mapema leo, Alhamisi ili kufanya tathmini ya mzunguko wa kwanza uliomalizika ikiwamo kutangaza tarehe ya kufunguliwa dirisha dogo la usajili pamoja na kuanza kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na Pemba.

## Oysterbay Queens kugeukia mastraika

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Oysterbay Queens, Juma Kweka, amekiangalia kikosi chake na kufunguka kuwa anahitaji kukiimarisha kwa kusajili washambuliaji wataokisaidia kufanya vizuri katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara inayoendelea msimu huu wa 2021/22.

Oysterbay Queens ambayo inashiriki ligi hiyo kwa mara ya kwanza, tayari imecheza mechi mbili na kupoteza zote ikiwamo kukubali kichapo cha mabao 8-0 dhidi ya Simba katika Uwanja wa Mo Simba Arena juzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kweka alisema michezo hiyo miwili imempa mwanga na kuona mapungufu yao mapema na sasa watayafanyia kazi mapema ikiwamo kufanya usajili washambuliaji.

Alisema nafasi zilizobaki beki na viungo, anaendelea kuwajenga na kuwapa mbinu kwenye mazoezi kwa sababu ana imani nao wanaweza kubadilika na kufanya vizuri.

"Timu yangu si mbaya sana, ukingalia wachezaji wangu wengi ni wageni pia hawana uzoefu katika Ligi Kuu, mechi mbili tumetengeneza nafasi lakini tumekosa mtu wa kumalizia na nimeliona hilo nalifanyia kazi kipindi hiki cha dirisha dogo," alisema Kweka.

Alisema anahitaji kufanyia kazi mapema ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo yao ya mbele ya ligi hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAPHINA HATASHINIKIZA JANUARI

WINGA wa Leeds United, Raphinha amekuwa akihusishwa na Liverpool na Bayern Munich, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 25, hatashinikiza kuhama Januari. ***(Mirror)***

### BARCA YAMTAKA AZPILICUETA

BARCELONA haijakata tamaa katika kujaribu kumsajili mlinzi wa Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32, na beki wa kati wa Denmark, Andreas Christensen mwenye miaka 25, kutoka Chelsea. ***(Sport)***

### EVERTON KUMSAJILI BARKLEY

EVERTON wamejadili uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 28, Ross Barkley kwa mkopo kutoka Chelsea wakati wa dirisha la uhamisho la Januari. ***(Telegraph)***

### DIGNE KUTUA CHELSEA

CHELSEA wanafikiria kujaribu kumsajili beki wa kushoto wa Everton, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ufaransa, huku timu hiyo ya Stamford Bridge ikimkosa beki wake, Ben Chilwell mwenye miaka 25 kwa kipindi kirefu kwa sababu ya jeraha la goti. ***(90 Min)***

### SCHICK AWINDWA EPL

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Czech, Patrik Schick mwenye umri wa miaka 25, analengwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England - akiwa anatazamwa na Arsenal, Everton, Manchester City, Tottenham na West Ham katika miezi ya hivi karibuni, lakini Bayer Leverkusen hawana haraka ya kumuuza mchezaji huyo ambaye yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2025. ***(90 Min)***

### UMTITI ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanapanga kumnunua beki wa kati wa Ufaransa, Samuel Umtiti, huku Barcelona wakitamani kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Marca)***

### NEWCASTLE YAMGEUKIA BARBOSA

NEWCASTLE pia wana nia ya kumleta mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Barbosa Januari, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, angependelea kusalia kule Flamengo. ***(Mirror)***

### INSIGNE AWANIWA TORONTO


MSHAMBULIAJI wa Italia, Lorenzo Insigne, ambaye mkataba wake na Napoli unakamilika msimu wa majira ya joto, anashawishiwa na ofa kutoka kwa Toronto FC. ***(Sky Sport Italia, via Football Italia)***

### DYBALA NA JUVE

JUVENTUS wanataka kubadilisha masharti ya kuongeza mkataba yaliyokubaliwa na mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, ambaye atakuwa huru kuondoka katika klabu hiyo mkataba wake wa sasa utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(La Gazzetta dello Sport, via Football Italia)***

### COOK KUTUA QPR

KLABU ya Queens Park Rangers iko mbele ya Nottingham Forest katika kujaribu kumsajili beki, Steve Cook mwenye umri wa miaka 30 kutoka Bournemouth. ***(Mail)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ATOA MSIMAMO MPYA HATIMA YAKE PSG

Hapana, sitajiunga na Real Madrid Januari, haitatokea, kwa asilimia 100 nitamaliza msimu nikiwa...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ameahidi hataondoka Paris Saint-Germain kwenda Real Madrid katika dirisha dogo la Januari.

Mbappe amebakiwa na miezi sita kwenye mkataba wake wa sasa na alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa 'Los Blancos' hao Agosti, lakini PSG walikataa kumuuza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amesema hana mpango wa kuondoka wakati wa dirisha dogo, na kwa sasa akili yake ni kutaka kushinda mataji akiwa na PSG.

"Hapana, sitajiunga na Real Madrid Januari," alisema Mbappe akiiambia CNN. "Kwa Januari haitatokea.

"Mimi nipo Paris Saint-Germain, nina furaha kubwa, na kwa asilimia 100 nitamaliza msimu nikiwa mchezaji wa PSG. Nitajitoa kwa kila kitu kushinda mataji yote nikiwa na Paris mwaka huu.

"Nitajitoa kwa hali na mali kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ligi. Na kuwapa raha mashabiki wote kwa sababu wanastahili hilo.

"Nina furaha kubaki. Hili ni jiji langu. Mimi ni Mfaransa. Nataka kushinda kila kitu msimu huu."

Miamba hao wa Ligue 1 wana matumaini straika huyo wa Ufaransa atakubali kusaini mkataba mpya, lakini wapo kwenye hatari ya kumpoteza akiwa mchezaji huru kama atakataa kuongeza mkataba.

PSG na Madrid watakutana kwenye mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16 na Mbappe amewahakikishia mashabiki yupo tayari kuisaidia timu hiyo.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME
MANCHESTER UTD
1.45 | 4.49 | 6.74
BURNLEY
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: KIPIGO LIVERPOOL SAHIHI



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amekubali Liverpool hawawezi kujilaumu kutokana na kipigo kutoka kwa Leicester City na amewaonya wachezaji wake kujifunza kutokana na kiwango kibovu walichoonyesha.

Wekundu hao walipoteza kwa bao 1-0 pale kwenye Uwanja wa King Power Jumanne na walishindwa kupunguza pengo la pointi sita dhidi ya vinara wa Ligi Kuu, Manchester City.

Liverpool ambao wamefunga mara mbili katika kila mechi kati ya 28 kwenye mashindano yote msimu huu, walishuhudia straika wao, Mohamed Salah akikosa penalti na Sadio Mane alipoteza nafasi nzuri ya kufunga.

Mchezaji wa zamani wa Everton, Ademola Lookman alifunga dakika tatu baada ya kuingia uwanjani akitokea benchi na kuwafanya Leicester kushinda mfululizo dhidi ya Liverpool.

Kikosi hicho cha Klopp kilipambana kurudisha bao hilo, lakini Leicester walionekana kuwa makini kulilinda.

"Kwa hakika Leicester walistahili ushindi," alisema Klopp akinukuliwa na Amazon Prime.

"Ulikuwa mchezo mgumu. Hatukuwa kwenye ubora wetu, hata kama tulikuwa na nafasi ya kutosha.

"Kile tulichofanya tukiwa na mpira hakikuwa sawa. Tulicheza mchezo mbaya, hivyo tulistahili kufungwa.

"Maamuzi yetu yalikuwa ya hovyo, pengine tulikosa nafasi na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Tulitakiwa kuwa na nafasi zaidi.

"Nafikiri tulianza vizuri, halafu tukamaliza kwa kucheza vibaya. Kuanzia hapo hatukuwa kwenye ubora wetu.

# Torres ajisifu kujiunga Barca

**BARCELONA, Hispania**

FERNANDO Torres anachukulia kujiunga na Barcelona kutoka Manchester City ni "hatua kubwa" katika maisha yake ya soka na anajiamini ataendelea kuimarika chini ya Xavi pale Camp Nou.

Barca ilithibitisha Jumanne kwamba imefikia makubaliano ya kumsaini Torres kutoka City kwa ada ya euro milioni 65.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania atatambulishwa rasmi Januari 3,mwakani lakini kutokana na majeraha aliyoyapata Oktoba yatamfanya asubiri kuanza kucheza hadi baadaye mwezi huo.

Torres ametumia miezi 18 kucheza pale kwenye dimba la Etihad baada ya kujiunga na Valencia kwa ada ya euro milioni 23 na alionyesha mchango wake kwenye mechi 43 alizoichezea City.

Yeye ni mmoja wa wachezaji wa City ambao walicheza angalau dakika 1,000 kwenye mashindano yote msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ana matumaini ya kuimarika zaidi hapo Barcelona. Akizungumza na tovuti ya Barcelona, Torres alisema: "Nina furaha kubwa kujiunga na Barca.

"Natumaini kuendelea kukua kama mchezaji wa soka na kuisaidia Barca kuwa moja ya timu bora duniani.

"Nina furaha kubwa kuwa hapa. Ni hatua kubwa kwa maisha yangu ya soka, kuendelea kukua, kufunga mabao. Nasubiria kwa hamu kujiunga nao rasmi."



LIVE IN PLAY

# KOCHA AZAM NA MATARAJIO KWA DUBE KUIVAA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi ambaye ni mwalimu wa makipa wa Azam FC, Iddi Abubakar, amesema anatarajia kuwapo na mabadiliko katika kikosi cha timu yake kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayopigwa Januari Mosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nyota ambao watasababisha mabadiliko makubwa katika kikosi hicho ni Bruce Kangwa, Nivere Tigere na Prince Dube ambao wataukosa mchezo huo na mingine ijayo kutokana na kuitwa kwenye timu ya Taifa ya Zimbabwe kuitumikia katika fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), zitakazofanyika nchini Cameroon.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo alisema hawana uhakika mkubwa kama watawakosa nyota hao kwa sababu wako kwenye mchujo.

Alisema endapo wachezaji hao watapenya katika mchujo na kujumuishwa katika kikosi kitakachoenda kucheza AFCON, hawataathirika kwa sababu tayari wamewaandaa vijana watakaochukuwa nafasi zao.

"Wakifanikiwa kuingia katika mchujo wa timu hiyo na kuwa miongoni mwa wachezaji watakaoicheze Zimbabwe kwenye AFCON, itatulazimu kufanya mabadiliko ya kikosi kuelekea mchezo wetu dhidi ya Azam FC," alisema kocha huyo.



Alisema wamejiandaa vizuri kwa kuwaandaa wachezaji wote kulingana na mahitaji ya mchezo huo ambao kwao ni muhimu kupata pointi kutokana na kuanza msimu huu kwa kusuasua.

Iddi alisema anatarajia mchezo wenye ushindani kwa kuwa timu zote mbili zimetoka kushinda mechi zao zilizopita.

Simba ambayo itakuwa mwenyeji wa mechi hiyo, mchezo uliopita iliibuka na ushindi wa mabao 4-1 ugenini dhidi ya KMC wakati Azam FC nayo ilipata ushinda kama huo dhidi ya Ruvu Shooting.

# Bwire alia na mwamuzi mechi KMC

**Na Dennis Fussi**

OFISA Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, amepaza sauti yake kwa kusema kwamba, waamuzi wanaua soka la Tanzania kutokana na maamuzi yao ya ovyo wanayoyatoa kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kauli hiyo ya Bwire ameitoa baada ya Ruvu Shooting kulazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 na KMC kwenye mchezo uliopigwa juzi Jumanne katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

KMC ilisawazisha bao dakika ya pili kwenye muda wa nyongeza kupitia kwa Charles Ilamfya na kuzifanya timu hizi kugawana pointi moja moja, wakati lile la Ruvu lilifungwa na Ally Kombo dakika ya 22.

Bwire anaona kwamba, mwamuzi wa mchezo huo aliongeza muda zaidi na kuwawezesha KMC kupata sare hiyo jambo ambalo amesema hawakutendewa haki.

"Siku zote tunalia na maamuzi ya waamuzi, leo (juzi) mwamuzi aliwaongezea muda zaidi KMC na wakasawazisha bao," alisema Bwire.

Aliongeza; "Mwamuzi alionyesha wazi kabisa kuibeba KMC, kwani baada ya kuongeza muda zaidi na lilipofungwa tu bao na yeye akamaliza mchezo, hii si sawa kabisa, waamuzi wanaua soka la Tanzania.

"Kwa maamuzi haya, kuna siku anaweza kutokea mtu akiwa na hasira na akafanya jambo la hatari sana. Kwa nini kila siku tunalia na waamuzi lakini hakuna hatua zinazochukuliwa?"

Kwa matokeo hayo, KMC imefikisha pointi 11 ikiwa katika nafasi ya 12 na Ruvu Shooting sasa ina pointi 10 katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo.




SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 30 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 3967 | Gold Coast Knights vs Melbourne Victory | 8.11 | 5.98 | 1.24 |
| 13:00 | 3772 | Yeni Malatyaspor vs Bandirmaspor | 1.66 | 3.62 | 4.53 |
| 14:00 | 5877 | Neroca FC vs Gokulam Kerala FC | 4.62 | 3.61 | 1.65 |
| 15:00 | 1328 | Gor Mahia vs Nairobi City Stars FC | 1.83 | 3.09 | 4.35 |
| 15:00 | 1358 | Bidco United vs Wazito | 2.46 | 2.79 | 2.99 |
| 15:00 | 1762 | Tusker vs Mathare United | 1.54 | 3.66 | 5.59 |
| 15:00 | 2123 | Konyaspor vs Umraniyespor | 1.57 | 3.80 | 5.01 |
| 15:00 | 3722 | Kayserispor vs Yeni Aksarayspor | 1.19 | 5.97 | 10.59 |
| 15:00 | 5518 | Kenya Commercial Bank vs Nzoia United | 1.48 | 3.95 | 5.78 |
| 15:00 | 5823 | Posta Rangers vs Kenya Police | 2.04 | 2.90 | 3.77 |
| 16:00 | 1705 | Shabab AL Amari vs Tubas | 2.13 | 3.27 | 3.08 |
| 16:00 | 2608 | Al Ain vs Ajman Club | 1.38 | 4.84 | 6.01 |
| 16:00 | 3226 | Rutsiro FC vs Gorilla FC | 2.08 | 2.93 | 3.61 |
| 16:00 | 3570 | Al Dhafra vs Al Nasr Dubai | 4.42 | 4.04 | 1.60 |
| 16:00 | 5451 | AS Kigali vs Mukura | 1.52 | 3.71 | 5.78 |
| 16:00 | 5988 | Namungo vs Biashara United | 1.94 | 2.90 | 4.16 |
| 17:00 | 2853 | Chennaiyin FC vs Bengaluru FC | 2.47 | 3.20 | 2.62 |
| 17:00 | 4241 | Sivasspor vs Ankaragucu | 1.71 | 3.51 | 4.33 |
| 17:00 | 5810 | Aizawl FC vs Mohammedan SC | 3.51 | 3.27 | 1.96 |
| 17:30 | 4815 | AL Qadsia vs Al Fehaheel | 1.23 | 5.19 | 10.57 |
| 18:00 | 5736 | Pacos F. U19 vs GIL Vicente U19 | 1.69 | 3.66 | 4.23 |
| 18:00 | 5834 | Raja Casablanca vs MAS Maghrib A Fes | 1.55 | 3.61 | 5.59 |
| 18:20 | 3495 | Al Khoor vs Qatar SC | 4.72 | 3.66 | 1.63 |
| 18:20 | 5522 | Al Arabi Doha SC vs Umm-Salal SC | 1.91 | 3.47 | 3.47 |
| 18:30 | 2344 | Al Wasl Dubai vs AL Urooba | 1.61 | 3.95 | 4.43 |
| 18:30 | 2397 | Gaziantep BB vs Bursaspor | 1.65 | 3.66 | 4.53 |
| 18:30 | 2604 | Baniyas vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 3.13 | 3.66 | 1.97 |
| 18:30 | 3677 | ES Bafing vs Sporting Gagnoa | 2.98 | 2.69 | 2.55 |
| 19:00 | 4497 | Shabab Alsamu vs Shabab AL Khaleel | 7.54 | 4.83 | 1.31 |
| 19:45 | 3707 | AL Tadamon vs Kazma SC | 5.78 | 4.72 | 1.40 |
| 20:00 | 1242 | Pacos Ferreira vs Santa Clara | 2.51 | 3.06 | 2.86 |
| 20:00 | 3524 | Atletico Saguntino vs CD Roda | 2.07 | 2.79 | 3.85 |
| 20:00 | 5737 | Deportivo Malacateco vs CSD Comunicaciones | 2.51 | 2.80 | 2.90 |
| 20:15 | 5982 | Olympique Khouribga vs FAR Rabat | 3.27 | 2.94 | 2.20 |
| 21:00 | 4594 | Besiktas vs Altay | 1.46 | 4.33 | 5.39 |
| 21:00 | 5442 | LYS Sassandra vs Club Omnisports de Korhogo | 2.40 | 2.79 | 3.08 |
| 22:00 | 1121 | CD Campos vs CD Binisalem | 2.02 | 3.28 | 3.33 |
| 22:00 | 2200 | FC Arouca vs Sporting Braga | 4.94 | 3.70 | 1.66 |
| 22:00 | 2510 | CD Manacor vs CF Soller | 1.73 | 3.37 | 4.43 |
| 22:30 | 2479 | Vitoria Setubal vs UD SantarÃƒÂ©m | 1.46 | 4.05 | 5.98 |
| 22:45 | 2383 | Nottingham vs Huddersfield | 1.96 | 3.33 | 3.72 |
| 22:45 | 2782 | Stoke City vs Derby | 1.66 | 3.33 | 5.68 |
| 22:45 | 3059 | Sunderland vs Sheffield Wed | 2.01 | 3.34 | 3.54 |
| 22:45 | 3895 | Bournemouth vs Cardiff | 1.60 | 3.77 | 5.29 |
| 22:45 | 5800 | Bristol City vs QPR | 2.84 | 3.28 | 2.37 |
| 23:15 | 3117 | Manchester Utd vs Burnley | 1.45 | 4.49 | 6.74 |

IJUAMAA - 31 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 5940 | Porto vs Benfica | 1.74 | 3.71 | 4.35 |
| 11:30 | 2750 | Sudeva Delhi FC vs Pailan Arrows | 1.51 | 3.70 | 5.96 |
| 14:00 | 1829 | Real Kashmir vs Kenkre FC | 1.43 | 4.26 | 6.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Desemba 30, 2021
Nipashe



## Mbappe atoa msimamo hatima PSG



Pablo

# PABLO ACHAMBUA KUNDI LA SIMBA CAF

### Asema malengo nusu fainali palepale, aonya ya Red Arrows, Asec Mimosas wembe mbele, ukuta...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikipangwa kundi lenye timu bora kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Mhispania Pablo Franco, amesema hiyo haiwezi kuondoa malengo yao ya kufika nusu fainali ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Katika droo iliyochezeshwa juzi jijini Cairo Misri, Simba imepangwa Kundi D pamoja na mabingwa wa mwaka 1998 wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Asec Mimosas ya Ivory Coast, Gendarmerie (USGN) ya Niger pamoja na mabingwa wa msimu wa 2019-20 wa Kombe la Shirikisho Afrika, RS Berkane ya Morocco.

Lakini Pablo amesema wakati anakabidhiwa mikoba ya kukinoa kikosi hicho, aliambiwa malengo yao ni kufika nusu fainali, jambo ambalo anaona ni wakati sasa wa kuanza maandalizi mapema kwa ajili ya michuano hiyo, kutokana na ratiba kuonyesha kwamba wataanzia nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Februari 13, mwakani dhidi ya Asec Mimosas.

Pablo alisema kadri wanavyosonga mbele katika michuano hiyo ndivyo ambavyo inazidi kuwa migumu, lakini wapo tayari kufanya maandalizi makubwa ili kuhakikisha wanafikia malengo yao.

"Unajua RS Berkane ni timu nzuri na ina mchezaji wetu nyota wa zamani, Clatous Chama, kwa hivyo tunajua haitakuwa mechi rahisi, lakini Asec nayo ni timu kongwe na ina uzoefu mkubwa katika michuano hii.

"Kwa upande wa Gendarmerie (USGN) nayo si timu ya kubeza hasa tukikumbuka mchezo uliopita dhidi ya Red Arrows, ulivyokuwa mgumu, hivyo hatutaidharau kwa namna yoyote, kila mchezo utakuwa kama fainali kwetu hadi tutimize malengo yetu," alisema Pablo aliyerithi mikoba ya Mfaransa Didier Gomes.

Kwa mujibu wa ratiba baada ya Simba kuikaribisha Asec Mimosas, itaifuata USGN Februari 20 na siku saba baadaye itaenda kuvaana na RS Berkane kabla ya Machi 13 kurejea nyumbani kurudiana na Wamorocco hao na kisha Machi 20 kuwafuata mabingwa mara 27 wa Ivory Coast kabla ya Aprili 22 kurudi Uwanja wa Benjamin Mkapa kuhitimisha hatua ya makundi dhidi ya Waniger, USGN.

**UBORA WA WAPINZANI; ASEC**

Kama ambavyo Pablo ameeleza ni wazi hakuna timu ya kubeza katika kundi hilo kwani zote licha ya kufuzu hatua hiyo, zinaendelea kufanya vizuri kwenye ligi za kwao.

Kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ivory Coast maarufu Ligue 1, Asec Mimosas ipo kileleni ikiwa na pointi 18 baada ya kushinda mechi zote sita ilizocheza hadi sasa kwenye ligi hiyo inayojumuisha timu 14, huku ikiwa imefunga mabao 12 na kuruhusu matatu tu. Timu inayoifuata ni Gagnoa ikiwa na alama 15 baada ya kupoteza mchezo mmoja.

**RS BERKANE**

Kwa upande wa Ligi Kuu Morocco maarufu kama Botola Pro 2021/22, hadi sasa ikiwa raundi ya 13, RS Berkane ipo nafasi ya sita ikiwa na pointi 19 baada ya kushinda mechi nne, sare saba, kupoteza mbili huku ikifunga mabao 14 na kuruhusu 11.

Msimamo wa ligi hiyo nchini Morocco unaongozwa na Wydad Casablanca yenye alama 32 kutokana na kushinda michezo 10 sare mbili na kupoteza mmoja. Timu inayofuata ni Raja Casablanca (pointi 27) FAR Rabat (23), Difaa El Jadida (20) na Jeunesse Sportive Soualem yenye pointi 19 sawa na RS Berkane lakini ikiwa na mabao mengi ya kufunga.

**GENDARMERIE**

US Gendarmerie kwenye Ligi Kuu Niger msimu huu ambayo nayo inashirikisha timu 14 na sasa ikiwa raundi ya nne, yenyewe imeshuka dimbani mara tatu, ipo nafasi ya sita ikiwa na pointi tano baada ya kushinda mechi moja na sare mbili, huku ikiwa imecheka na nyavu mara nne na kuruhusu mabao mawili. Timu iliyopo kileleni ni Douanes Niamey ikiwa na pointi 10, ikifuatiwa na Nigelec, Police, Sahel huku ASGNN ikiwa na alama sita, lakini timu hizo kila moja zikiwa zimecheza mechi nne.

**SIMBA**

Tofauti ya Simba na Asec Mimosas kwenye matokeo ya ndani inaweza kuwa ni sare tatu ambazo 'Wekundu wa Msimbazi' hao wamezipata hadi sasa katika michezo yao tisa, wakati huu ikiwa na pointi 21 katika nafasi ya pili nyuma ya Yanga yenye alama 26 zilizotokana na michezo 10.

Simba ina mabao 12 ya kufunga na matatu ya kufungwa kama ilivyo kwa Asec Mimosas, lakini yenyewe idadi hiyo ikitokana na mechi sita ilizocheza kwenye ligi ya kwao hadi sasa.

## Nabi ataja mbadala wa Bangala, Djuma

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukiri ugumu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amebadilisha gia ya mazoezi kwa kuhakikisha kila mchezaji anakuwa na utimamu mzuri wa mwili ili kuwa tayari kwa michezo iliyopo mbele yao.

Hatua hiyo ni baada ya baadhi ya nyota wa Yanga akiwamo Yanick Bangala, Mukoko Tunombe na Djuma Shabani, ambao wameitwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya DR Congo pamoja kipa Djigui Diarra (Mali), kwenda kuzitumikia timu zao kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika nchini Cameroon.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema anaamini wana wachezaji bora, hivyo kukosekana kwa nyota hao watatu, tayari wengine wanaweza kucheza nafasi zao.

Alisema kurejea kwa Balama Mapinduzi na Dickson Ambundo, kumeifanya timu hiyo kuwa na kikosi kipana na kila mmoja wao kuanza kufanyia kazi majukumu wanayopewa mazoezini.

"Kama tutawakosa wachezaji walioitwa katika timu zao za taifa, haitakuwa kikwazo kikubwa kwetu kwa sababu tuna nyota wengi bora na kuna wale waliokuwa majeruhi wako fiti na wamerejea vizuri matarajio yetu watatusaidia katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Nabi.

Alisema ukiwa na wachezaji wengi bora, unatakiwa kutafuta namna ya kuwapa nafasi ya kucheza hali ambayo ataanza nao katika mechi dhidi ya Dodoma Jiji FC na katika michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar.

9 770856 541002 >